# MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA

TMDA
Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

# TAARIFA YA UTENDAJI KAZI YA MWAKA 2024/25

**(Julai 2024 – Juni 2025)**

Julai, 2025





# YALIYOMO

**YALIYOMO** ........ i
**Barua ya Kuwasilisha.** ........ ii
**Maelekezo ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri (MAB).** ........ iii
**Maelezo ya Mkurugenzi Mkuu.** ........ iv

**1.0 UTANGULIZI** ........ 1
1.1.1 Hatua ya Utekelezaji wa Kila Lengo Mkakati. ........ 2
1.1.2 Kuhakikisha Usalama, Ubora na Ufanisi wa Dawa na Vipukusi ........ 2
1.1.3 Tathmini na Usajili wa Dawa ........ 2
1.1.4 Tathmini na Usajili wa Dawa za Binadamu ........ 3
1.1.5 Tathmini na Usajili wa Dawa za Mifugo ........ 3
1.1.6 Tathmini ya Usajili wa Dawa za Mitishamba ........ 4
1.1.7 Tathmini ya Usajili wa Vipukusi (Antiseptics/ Disinfectants) ........ 4
1.1.8 Tathmini ya Maombi ya Matangazo ya Dawa ........ 4
1.1.9 Tathmini na Usajili wa Majaribio ya Dawa (Clinical Trials) ........ 6
1.1.10 Usajili na Utoaji wa Vibali vya Maeneo ya Biashara ya Dawa na Vipukusi. ........ 7

**1.2 UKAGUZI WA MAENEO YA BIASHARA ZA DAWA NA VIPUKUSI** ........ 8
1.2.1 Maeneo ya Biashara za Dawa, Vipukusi na Majaribio ya Dawa ........ 8
1.2.2 Ukaguzi wa Viwanda vya Kutengeneza Dawa Ndani ya Nchi ........ 9
1.2.3 Ukaguzi Maalum wa Dawa Tiba Zenye Asili ya Kulevya ........ 9
1.2.4 Ukaguzi wa Majaribio ya Dawa ........ 10
1.2.5 Udhibiti wa Uingizaji Nchini na Usafirishaji nje ya Nchi wa Bidhaa za Dawa ........ 10
1.2.6 Kupokea na Kutathmini Taarifa za Matukio Makubwa ya Kiafya (Serious Adverse Events - SAE) Yanayotokea Katika Majaribio ya Dawa ........ 10
1.2.7 Ufuatiliaji wa Usalama wa Dawa na Chanjo ........ 11
1.2.8 Ufuatiliaji wa Ubora wa Dawa na Chanjo katika Soko (Post Marketing Surveilance - PMS) 16

**2.0 KUHAKIKISHA USALAMA, UBORA NA UFANISI WA VIFAA TIBA NA VITENDANISHI** ........ 25
2.1.1 Usajili wa Vifaa Tiba na Vitendanishi ........ 25
2.1.2 Tathmini na Usajili wa Vifaa Tiba ........ 26
2.1.3 Tathmini na Usajili wa Vitendanishi ........ 28
2.1.4 Tathmini na Usajili wa Maombi Mengine ya Vifaa Tiba ........ 28
2.1.5 Tathmini na Usajili wa Maombi Mengine ya Vitendanishi ........ 29
2.1.6 Tathmini ya Maombi ya Utambuzi wa Vifaa Tiba na Vitendanishi ........ 29
2.1.7 Usajili wa Maeneo na Utoaji wa Vibali vya Biashara ya Vifaa Tiba na Vitendanishi ........ 31
2.1.8 Ukaguzi wa Viwanda na Maeneo ya Biashara za Vifaa Tiba, Vitendanishi na Gesi Tiba ........ 31
2.1.9 Ukaguzi wa Viwanda vya Kati, Vidogo na Meneo ya Biashara ........ 32
2.2.0. Ukaguzi wa Viwanda Vikubwa vya Ndani ........ 32
2.2.1 Ukaguzi wa Viwanda vya Kutengeneza Gesi Tiba ........ 33
2.2.2 Ukaguzi wa Viwanda vya Vifaa Tiba na Vitendanishi Nje ya Nchi ........ 33
2.2.3 Udhibiti wa uingizaji nchini na usafirishaji nje ya nchi wa vifaa tiba na vitendanishi ........ 33

2.2.4 Ufuatiliaji wa Usalama wa Vifaa Tiba na Vitendanishi ....34
2.2.4.1 Ufuatiliaji Ubora na Ufanisi wa Vifaa Tiba wa Vitendanishi Kupitia Upimaji wa Toleo kwa Toleo Kabla ya Kusambazwa ....34
2.2.4.2 Utekelezaji wa Mpango wa Ufuatiliaji wa Ubora na Ufanisi wa Vifaa Tiba na Vitendanishi *(PMS Programme)*....36
2.2.4.3 Ufuatiliaji wa Matukio Yatokanayo na Matumizi ya Vifaa Tiba na Vitendanishi (Vigilance)....37
2.2.4.4 Utekelezaji wa Mpango wa Ufuatiliaji Ubora na Ufanisi na Vifaa Tiba Vikubwa Katika Soko....39
2.2.4.5 Hali ya Soko la Vifaa Tiba na Vitendanishi Nchini ....39
2.2.4.6 Kazi za Mradi wa Breedime ....40
2.2.4.7 Kuandaa Mwongozo wa *"Perfomance Evaluation na Protocols"*....40
2.2.4.8 Kupitia "Performance Evaluation Data" Katika Maombi ya Usajili....41
2.2.4.9 Uteketezaji wa Bidhaa Zisizokidhi Viwango ....41
2.3.0 Kuimarisha Udhibiti wa Bidhaa za Tumbaku ....42

**3.0 KUBORESHA HUDUMA ZA MAABARA .... 43**
**3.1 Uchunguzi wa Sampuli za Bidhaa Zinazodhibitiwa .... 43**
**3.2 Uchunguzi wa Sampuli za Dawa Dar es salaam.... 43**
**3.3 Uchunguzi za Sampuli za Vifaa Tiba na Vitendanishi.... 44**
**3.4 Uchunguzi wa Sampuli za Dawa na Vipukusi Mwanza .... 45**
**3.5 Uchunguzi wa Awali wa Dawa Katika Maabara Hamishika.... 46**
**3.6 Utekelezaji wa Mifumo ya Ubora wa Utendaji Kazi (ISO/IEC 17025:2017 na WHO/GP-PQCL) ....47**
**3.7 Ugezi, Matengenezo na Ununuzi wa Vifaa, Kemikali na Mahitaji Mengine ya Maabara 47**

**4.0 KUIMARISHA UTOAJI ELIMU KWA UMMA NA KUBORESHA HUDUMA KWA WATEJA .... 48**
**4.1 Utoaji Elimu kwa Umma .... 48**
**4.2 Kuboresha Huduma kwa Wateja .... 50**

**5.0 KUIMARISHA UWEZO WA TAASISI KUTOA HUDUMA ZA UDHIBITI .... 51**
**5.1 Usimamizi wa Rasilimali Watu .... 51**
5.1.1 Idadi Ya Watumishi .... 51
5.1.2 Utekelezaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji Kazi Katika Utumishi wa Umma.... 51
5.1.3 Mafunzo kwa vitendo.... 51
5.1.4 Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini..... 52
5.1.5 Ushiriki wa Michezo Kwa Watumishi.... 52
5.1.6 Taarifa ya Utendaji wa Kamati Mbalimbali.... 52
5.1.7 Maboresho ya Muundo wa Maendeleo ya Watumishi na Muundo wa Mishahara .... 53
5.1.8 Uhakiki Mifumo na Usimamizi wa Vihatarishi.... 53
**5.2 MIPANGO, UFUATILIAJI NA TATHMINI.... 54**
**5.3 TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA).... 55**
**5.4 UKAGUZI WA NDANI.... 57**

**5.5 MANUNUZI NA UGAVI ........ 57**
5.5.1 Utangulizi ........ 57
5.5.2 Utekelezaji wa Mpango wa Ununuzi ........ 57
5.5.3 Kuratibu Vikao vya Bodi ya Zabuni ........ 58
5.5.4 Usimamizi wa Mikataba ........ 58
5.5.5 Usimamizi wa Mali za Mamlaka ........ 58
5.5.6 Mafanikio Katika Kutekeleza Majukumu Kwa Mwaka 2024/2025 ........ 59
**5.6 HUDUMA ZA SHERIA ........ 60**
5.6.1 Bodi ya Ushauri ya Wizara ya Afya kwa TMDA (MAB) ........ 60
5.6.2 Kanuni Zilizoandaliwa ........ 61
5.6.3 Mapendekezo na Kurekebisha Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura ya 219 ........ 61
5.6.4 Mikataba ........ 61
5.6.5 Randama za Makubaliano (MoU) ........ 62
5.6.6 Utekelezaji wa Sheria Mbalimbali ........ 63
**5.7 MAPATO NA MATUMIZI ........ 63**
5.7.1 Mapato ya Mwaka 2024/2025 ........ 63

**6.0 KUTOA HUDUMA KWA WAATHIRIKA WA VIRUSI VYA UKIMWI NA WENYE MAGONJWA YASIYOAMBUKIZA ........ 64**

**7.0 KUIMARISHA NA KUTEKELEZA KWA UFANISI MKAKATI WA TAIFA WA KUPAMBANA NA KUZUIA RUSHWA ........ 65**

**8.0 KUBORESHA MASUALA YA JINSIA NA MAZINGIRA ........ 66**

**9.0 MAENEO YATAKAYOPEWA KIPAUMBELE 2025/2026 ........ 67**
**9.4 HITIMISHO ........ 68**

**10.0 INDEPENDENT REPORT OF THE CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL ........ 69**

# Barua ya Kuwasilisha



**Mhe.Jenista Mhagama (MB),**
Waziri wa Afya,
Mji wa Serikali,
Barabara ya Afya,
S.L.P 743,
11478 Dodoma.



**Dkt.Seif Shekalaghe,**
Katibu Mkuu,
Wizara ya Afya,
Mji wa serikali,
S.L.P 743,
40478 Dodoma.

Mhe. Waziri,

Kwa niaba ya wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Wizara ya Afya kwa TMDA, ninayo heshima kubwa kuwasilisha kwako Taarifa ya Utendaji Kazi ya Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) kwa kipindi cha mwaka 2024/25.

Taarifa hii imeeleza hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa shughuli za udhibiti wa ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwa lengo la Kulinda Afya ya Jamii na Mazingira.

Nawasilisha.



**Dkt. Seif Shekalaghe**
**Katibu Mkuu (Afya)**

# Maelezo ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri (MAB)



**Mwaka 2024/25 ni mwaka wa nne wa utekelezaji wa Mpango mkakati wa TMDA wa miaka mitano (2021/22-2025/26) wenye lengo la kuimarisha utekelezaji wa shughuli za kudhibiti usalama, ubora na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi.**

Katika kipindi hiki, TMDA imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kisheria ya kudhibiti usalama, ubora na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwa lengo la kulinda afya ya jamii na mazingira. Aidha, Mamlaka imeendelea kutekeleza jukumu la udhibiti wa bidhaa za tumbaku lililokasimishwa Wizara ya Afya ambapo Bodi imeendelea kutoa miongozo na usimamizi wa kimkakati ili kuhakikisha majukumu haya yanatekelezwa kwa ufanisi na kwa kuzingatia matakwa ya sheria.

Katika kuimarisha utoaji huduma, TMDA imeendelea kutekeleza matakwa ya mifumo bora ya utendaji kazi (Quality Management System) na hivyo kuendelea kushikilia cheti cha ithibati kwa kiwango cha ISO 9001:2015. Huduma zimekuwa zikitolewa kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa katika Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa mwaka 2020, jambo lililochangia kuongeza uwazi, uwajibikaji na kuridhika kwa wadau.

Kwa kutambua umuhimu wa maamuzi ya kisayansi katika udhibiti, Mamlaka imeendelea kuwekeza katika kuimarisha miundombinu na vifaa vya maabara pamoja na kuwajengea uwezo wataalamu wake. Hatua hii imeongeza ufanisi katika uchunguzi na upimaji wa bidhaa zinazodhibitiwa, na hivyo kuimarisha shughuli za udhibiti.

Kwa ujumla Bodi imeridhishwa na namna Mamlaka ilivyoendelea kusimamia rasilimali zake kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za kiutendaji. Hesabu za fedha kwa kipindi kinachoishia Juni, 2025 zimeandaliwa kwa mujibu wa matakwa ya kisheria na ziko tayari kwa ukaguzi wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Katika kuendeleza ushirikishwaji wa wadau, TMDA imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu yake na matakwa ya Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba Sura, 219 kupitia mihadhara, vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Juhudi hizi zimeongeza uelewa wa wadau na kuchochea ushirikiano katika kuhakikisha bidhaa zilizopo katika soko zinakidhi vigezo vya usalama, ubora na ufanisi.

Kwa niaba ya Bodi ya Ushauri, napenda kumpongeza Mkurugenzi Mkuu, Menejimenti na watumishi wote wa TMDA kwa weledi, uadilifu na kujituma katika kutekeleza majukumu yao. Aidha, ninatoa shukrani za dhati kwa Wizara ya Afya, wadau wa sekta na wananchi kwa ushirikiano wao.

Bodi ya Ushauri itaendelea kutoa maelekezo na ushauri kwa Menejimenti ya TMDA na Wizara ya Afya ili kuhakikisha kuwa dawa, vifaa tiba na vitendanishi vinavyopatikana katika soko la Tanzania ni salama, bora na vyenye ufanisi.

**Bw. Eric Shitindi**
**Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri**

# Maelezo ya Mkurugenzi Mkuu



**Taarifa hii ya utendaji kazi inaainisha hatua iliyofikiwa na Mamlaka katika utekelezaji wa kazi na majukumu yake ya kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi nchini kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Juni, 2025. Aidha, maeneo yanayohitaji kupewa kipaumbele katika mwaka ujao wa fedha yameanishwa.**

Huu ni mwaka wa nne wa utekelezaji wa Mpango Mkakati wa TMDA wa miaka mitano (2021/22-2025/26) wenye malengo mkakati tisa (9) ambapo kumekuwa na mafanikio makubwa katika utekelezaji wake.

Katika kuhakikisha usalama, ubora na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi, Jumla ya maombi 2,098 ya usajili wa dawa za binadamu yalipokelewa na 1927 (91.8%) kutathminiwa ambapo maombi 1,121 (58%) yaliidhinishwa. Aidha, maombi 234 ya usajili wa dawa za mifugo yalipokelewa na 229 (97.8%) kutathminiwa na maombi 192 (83.8) yalikidhi vigezo na kuidhinishwa.

**Huu ni mwaka wa nne wa utekelezaji wa Mpango Mkakati wa TMDA wa miaka mitano (2021/22-2025/26) wenye malengo mkakati tisa (9)**

Vilevile, jumla ya Maombi 710 ya usajili (443 vifaa tiba na 267 vitendanishi) yalipokelewa ambapo maombi 681 sawa na 95.9% yalitathminiwa na maombi 255 kuidhinishwa. Idadi hii ya maombi ya usajili wa vifaa tiba na vitendanishi yaliyofanyiwa tathmini ni ongezeko la maombi 356 ikilinganishwa na maombi 325 yaliyoidhinishwa mwaka 2023/24.

Aidha, maombi 469 ya usajili wa maeneo ya biashara yalipokelewa katika kipindi tajwa ambapo maombi yote 469 yalifanyiwa kazi na kati ya hayo maeneo 447 (92%) yalisajiliwa na hivyo kupewa vibali vya biashara. Maeneo yasiokidhi vigezo vya usajili wamiliki walipatiwa maelekezo ya kuboresha maeneo husika.

Mamlaka pia ilipokea maombi 15,745 ya vibali vya kuingiza bidhaa nchini na 1,237 vya kusafirisha bidhaa nje ya nchi. Kati ya hayo, maombi 14,377 ya kuingiza bidhaa nchini na 1,157 ya kusafirisha bidhaa nje ya nchi yalikidhi vigezo na vibali kutolewa. Aidha, vibali 11,362 vya kuingiza bidhaa nchini na 495 vya kusafirisha bidhaa nje ya nchi vilikaguliwa katika vituo mbalimbali vya forodha.

Mamlaka ilifanya ukaguzi wa viwanda na maeneo 15,540 yanayoendesha biashara ya bidhaa zinazodhibitiwa na Mamlaka ambapo maeneo 13,026 sawa na 87% yalikidhi vigezo. Kiwango hiki cha kukidhi vigezo vya viwanda na maeneo ya biashara kinatoa picha kuwa bidhaa zinazalishwa na kuuzwa katika mazingira bora na salama kwa watumiaji.

> **Mamlaka ilitumia jumla ya TZS 54.3 bilioni sawa na 91% ya bajeti ya matumizi iliyopangwa kwa mwaka huu.**

> **Kwa ujumla TMDA imetekeleza kwa ufanisi na mafanikio makubwa malengo mkakati yaliyoanishwa katika mpango wa miaka mitano**

Kwa upande wa upimaji sampuli katika maabara, jumla ya sampuli 1,940 za dawa, vifaa tiba, vitendanishi na vipukusi zilipokelewa. Vilevile, kulikuwa na sampuli tano (5) ambazo ni baki kutoka mwaka 2023/2024. Hivyo kufanya jumla ya sampuli kuwa 1,945. Sampuli 1,820 sawa na 93.6% zilifanyiwa uchunguzi ambapo sampuli 1,694 (93.1%) zilifaulu.

Elimu kwa umma ilitolewa kwa makundi mbalimbali ya wananchi pamoja na kutangaza huduma za Mamlaka kupitia njia mbalimbali za uelimishaji. Njia zilizotumika ni pamoja na kufanya mihadhara, matangazo na vipindi vya runinga na redio pamoja na kushiriki katika maonesho mbali mbali ambapo zaidi ya washiriki 115,129 walifikiwa,

Kuhusu usimamizi wa rasilimali, Jumla ya TZS 61.6 bilioni zilikusanywa sawa na 103% ya bajeti ya makusanyo ya TZS 59.6 billoni ya mwaka wa fedha 2024/2025.

Kati ya fedha hizo TZS 47.7 Bilioni (109%) ni kutoka kwenye vyanzo vya ndani, TZS 6.4 bilioni ni mchango wa Serikali kuu na TZS 6.4 bilioni ni fedha za Washirika wa Maendeleo. Mamlaka ilitumia jumla ya TZS 54.3 bilioni sawa na 91% ya bajeti ya matumizi iliyopangwa kwa mwaka huu.

Kwa ujumla TMDA imetekeleza kwa ufanisi na mafanikio makubwa malengo mkakati yaliyoanishwa katika mpango wa miaka mitano sambamba na lengo mtambuka la kutekeleza Mkakati wa Taifa wa kupambana na kuzuia rushwa.

Nachukua nafasi hii kuishukuru serikali ya awamu ya sita chini ya Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) kwa usimamizi na sera nzuri zilizoiwezesha TMDA kufanya shughuli za udhibiti kwa umahiri na ufanisi mkubwa jambo lililopelekea kuimarisha afya na ustawi wa jamii.

Shukrani za pekee pia ni kwa Wizara ya afya kupitia Waziri wa Afya, Katibu Mkuu Afya na wajumbe wote wa bodi ya ushauri ambapo kupitia miongozo na maelekezo, TMDA imeendelea kuwa chombo cha kutumainiwa na jamii.

Vile vile nawapongeza watumishi wote kwa kufanya kazi kwa bidii, juhudi na maarifa ikiwa ni pamoja na kujituma katika kufikia malengo mkakati ya taasisi.

Mwisho nawashukuru wadau mbali mbali walioshirikiana na TMDA katika kutekeleza shughuli za udhibiti hasa vyombo vya habari, Washirika wa Maendeleo, taasisi mbali mbali za serikali, wateja wote wa taasisi na wananchi kwa jumla ambao kwa umoja wao wamekuwa sehemu ya mafanikio haya.

**Dkt. Adam M. Fimbo**
**Mkurugenzi Mkuu**

01

## Uwazi

Operate in a fully transparent manner and communicate openly and timely to the relevant stakeholders

02

## Uwajibikaji

Accountable for actions and outcomes

03

## Kumjali mteja

Always treat customers and colleagues with courtesy and be responsive, timely and proactive to meet their needs

04

## Ubunifu

Enhance innovation in service delivery

05

## Kufanya kazi kwa ushirikiano

Support one another, work cooperatively and respect one another's views

06

## Uaminifu

To uphold highest standards of conduct and commitments while acting in the best interest of the country

07

## Ubora

Strive to deliver the best services to the customers with utmost professionalism

# TAARIFA YA UTENDAJI KAZI YA MWAKA 2024/25

(Julai 2024 – Juni 2025)



## 1.0 UTANGULIZI

Katika kipindi cha mwaka 2024/25, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) iliendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Mpango Kazi na Bajeti ya mwaka 2024/25 iliyoidhinishwa. Taarifa hii inaainisha kazi zilizotekelezwa kwa kipindi tajwa kwa kuzingatia malengo mkakati tisa (9) ya Mpango Mkakati wa Mamlaka (2021/22 - 2025/26) ambayo ni: -

- Kuhakikisha usalama, ubora na ufanisi wa dawa na bidhaa zinazohusiana;
- Kuhakikisha usalama, ubora na ufanisi wa vifaa tiba na vitendanishi;
- Kuimarisha udhibiti wa bidhaa za tumbaku;
- Kuboresha huduma za maabara;
- Kuimarisha utoaji elimu kwa umma na kuboresha huduma kwa wateja;
- Kuimarisha uwezo wa Mamlaka katika kutoa huduma za udhibiti.
- Kupunguza maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na kuboresha huduma kwa waathirika wa UKIMWI na wenye magonjwa yasiyoambukiza;
- Kuimarisha na kutekeleza kwa ufanisi Mkakati wa Taifa wa kupambana na kuzuia rushwa; na
- Kuboresha masuala ya jinsia na mazingira

### 1.1.1 Hatua ya Utekelezaji wa Kila Lengo Mkakati

Kazi zilizotekelezwa na TMDA katika kipindi cha mwaka 2024/25 kwa mujibu wa Mpango Kazi na Bajeti ni kama ilivyoainishwa katika vipengele 1.2 – 8.0.

### 1.1.2 Kuhakikisha Usalama, Ubora na Ufanisi wa Dawa na Vipukusi

Mamlaka ina jukumu la kulinda afya za wananchi dhidi ya athari ambazo zinaweza kujitokeza kutokana na matumizi ya dawa na vipukusi. Hii ni pamoja na kufanya usajili na ukaguzi wa bidhaa husika, kufuatilia madhara yatokanayo na dawa na bidhaa zinazohusiana ikiwa ni pamoja na kufuatilia ubora na usalama wa bidhaa hizo katika soko. Katika kipindi hiki, Mamlaka ilitekeleza kazi za lengo mkakati tajwa kama zilivyoainishwa katika vipengele 1.2.3 – 1.4.0

### 1.1.3 Tathmini na Usajili wa Dawa

Jumla ya maombi 2,044 (mapya 1,082 na huisha 962) yalipokelewa sawa na 114% ya lengo la maombi 1,796. Vilevile, maombi 1,419 ya mabadiliko yalipokelewa sawa na 148% ya lengo la maombi 952.

Kuvukwa kwa lengo kwa upande wa maombi ya usajili wa dawa kumechangiwa na TMDA kuwa katika ngazi ya tatu (WHO - Maturity Level 3) katika mifumo ya udhibiti wa dawa kwa mujibu wa Shirika la Afya Dunia (WHO). Aidha, kutofikiwa kwa lengo kwa upande wa vipukusi kumechangiwa na kudhibitiwa kwa ugonjwa wa UVIKO -19. Pamoja na kupokea maombi mapya ya usajili, kuhuisha na mabadiliko, Mamlaka pia ilipokea majibu ya hoja 1,527 na hivyo kufanya jumla ya maombi yaliyopokelewa kuwa 4,990.

Vilevile, kulikuwa na salio la maombi 668 (mapya 329, kuhuisha 13, mabadiliko 142 na hoja 184) kutoka mwaka uliopita 2023/2024, hivyo kufanya jumla ya maombi yote yaliyokuwepo kuwa 5,658 ambapo jumla ya maombi 5,024 sawa na 89% ya maombi yote yaliyokuwepo yalifanyiwa tathmini.

Mchanganuo wa matokeo ya tathmini kwa aina mbalimbali za maombi ya usajili wa dawa ni kama yalivyoainishwa katika dondoo 1.2.4.-1.2.8.

**2,044**
Maombi yalipokelewa

**1,419**
Maombi ya mabadiliko

**1,527**
Majibu ya hoja

**668**
Salio la maombi

**5,024**
maombi yaliyofanyiwa tathmini



### 1.1.4 Tathmini na Usajili wa Dawa za Binadamu

Kati ya maombi 2,098, maombi 1,927 (mapya 1,099 na huisha 828) yalifanyiwa tathmini sawa na 92%. Maombi yaliyotathminiwa katika kipindi hiki ni ongezeko la maombi 605 ukilinganisha na maombi 1322 yaliyofanyiwa tathmini katika kipindi kama hiki mwaka 2023/24. Kati ya maombi yaliyotathminiwa, maombi 1,121 (mapya 536 na huisha 585) yaliidhinishwa, na maombi 51 yalikataliwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kubainika kughushi taarifa za usajili (maombi 48), kushindwa kufanya majaribio ya ulinganifu (bioequivalence) kwa kipindi cha miaka saba (7) (ombi 1), dawa kutokidhi vigezo vya ubora (ombi 1). Mchanganuo wa tathmini na usajili wa dawa za binadamu umeainishwa kwenye **Jedwali Na. 1:**

Vilevile, kati ya maombi mengine 2,946, maombi 2,831 (Mabadiliko 1,334 na hoja 1,497) sawa na 96 %yalifanyiwa tathmini. Maombi yaliyotathminiwa ni ongezeko la maombi 682 ukilinganisha na maombi 2,149 yaliyofanyiwa tathmini mwaka 2023/24. Kati ya maombi yaliyotathminiwa maombi 814 ya mabadiliko yaliidhinishwa. Mchanganuo wa tathmini ya maombi mengine umeainishwa kwenye **Jedwali Na. 2.**

### 1.1.5 Tathmini na Usajili wa Dawa za Mifugo

Kati ya maombi 234, maombi 229 (mapya 137 na huisha 92) yalifanyiwa tathmini sawa na 98%. Maombi yaliyotathminiwa katika kipindi hiki ni ongezeko la maombi 91 ukilinganisha na maombi 138 yaliyofanyiwa tathmini katika kipindi kama hiki mwaka 2023/24. Kati ya maombi yaliyotathminiwa, maombi 192 (mapya 132 na huisha 60) yaliidhinishwa, na maombi 7 yalikuwa na hoja. Mchanganuo wa tathmini na usajili wa dawa za mifugo umeainishwa kwenye **Jedwali Na. 1.**

Vilevile, kati ya maombi mengine 280, maombi 243 (mabadiliko 34 na hoja 209) yaliyokuwepo yalifanyiwa tathmini. Maombi yaliyotathminiwa ni ongezeko la maombi 55 ukilinganisha na maombi 188 yaliyofanyiwa tathmini mwaka 2023/24. Kati ya maombi mengine yaliyotathminiwa maombi saba (7) yaliidhinishwa. Mchanganuo wa tathmini ya maombi mengine umeainishwa kwenye **Jedwali Na. 2.**

**Dawa za Mitishamba**
Maombi 25
Maombi 11 yalifanyiwa tathmini
Maombi 25 mengine yalifanyiwa tathmini
Maombi 4 yaliidhinishwa

**Usajili wa Vipukusi**
Maombi 29
Maombi 26 yalifanyiwa tathmini
Maombi mengine 24 yalifanyiwa tathmini
Maombi 2 yaliidhinishwa

### 1.1.6 Tathmini ya Usajili wa Dawa za Mitishamba

Kati ya maombi 25, maombi 11 (mapya 10 na huisha 1) yalifanyiwa tathmini sawa na 44%. Maombi yaliyotathminiwa katika kipindi hiki ni ongezeko la ombi moja (1) ukilinganisha na maombi 10 yaliyofanyiwa tathmini katika kipindi kama hiki mwaka 2023/24. Kati ya maombi yaliyotathminiwa, maombi mapya 8 yaliidhinishwa, na hakukuwa na maombi yaliyokataliwa. Tathmini ya maombi 14 yaliyosalia inaendelea. Mchanganuo wa tathmini na usajili wa dawa za mitishamba umeainishwa kwenye **Jedwali Na. 1.**

Vilevile, kati ya maombi mengine 27, maombi 25 (mabadiliko 8 na hoja 17) yalifanyiwa tathmini. Maombi yaliyotathminiwa ni ongezeko la maombi 19 ukilinganisha na maombi yaliyofanyiwa tathmini mwaka 2023/24. Kati ya maombi yaliyotathminiwa maombi 4 ya mabadiliko yaliidhinishwa.

### 1.1.7 Tathmini ya Usajili wa Vipukusi *(Antiseptics/ Disinfectants)*

Kati ya maombi 29, maombi 26 (24 mapya, 2 huisha) yalifanyiwa tathmini sawa na 90%. Maombi yaliyotathminiwa katika kipindi hiki ni pungufu ya maombi 19 ukilinganisha na maombi 45 yaliyofanyiwa tathmini katika kipindi kama hiki mwaka 2023/24. Upungufu unatokana na idadi ndogo ya maombi yaliyopokelewa. Kati ya maombi yaliyotathminiwa, maombi 7 mapya yaliidhinishwa, na hakukuwa na maombi yaliyokataliwa. Mchanganuo wa tathmini na usajili wa vipukusi umeainishwa kwenye **Jedwali Na. 1.**

Vilevile, maombi yote mengine 24 (mabadiliko 6 na hoja 18) yalifanyiwa tathmini. Maombi yaliyotathminiwa ni ongezeko la maombi 20 ukilinganisha na maombi 4 yaliyofanyiwa tathmini mwaka 2023/24.

Kati ya maombi mengine yaliyotathminiwa maombi 2 yaliidhinishwa.

### 1.1.8 Tathmini ya Maombi ya Matangazo ya Dawa

Kati ya maombi 555, maombi 548 mapya yalifanyiwa tathmini sawa na 99%. Maombi yaliyotathminiwa katika kipindi hiki ni ongezeko la maombi 123 ukilinganisha na maombi 425 yaliyofanyiwa tathmini katika kipindi kama hiki mwaka 2023/24. Kati ya maombi yaliyotathminiwa, maombi 488 mapya yaliidhinishwa, na hakukuwa na maombi yaliyokataliwa.Mchanganuo wa tathmini na usajili wa vipukusi umeainishwa kwenye **Jedwali Na. 1:.**

**Jedwali Na. 1: Idadi ya Maombi ya Usajili wa Bidhaa za Dawa na Majaribio ya Dawa.**

| Na. | Bidhaa | Maelezo | Baki ya juni 2023 | Pokelewa | Jumla | Tathminiwa | Idhinishwa | Kataliwa | Baki |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Dawa za Binadamu | Mapya | 317 | 908 | 1225 | 1999 | 536 | 51 | 246* |
| | | Huisha | 0 | 873 | 873 | 828 | 585 | 0 | 45 |
| | | **Jumla Ndogo** | **317** | **1,781** | **2098** | **1,927** | **1,121** | **51** | **291** |
| 2. | Dawa za Mifugo | Mapya | 12 | 125 | 137 | 137 | 132 | 0 | 0 |
| | | Huisha | 13 | 84 | 97 | 92 | 60 | 0 | 5 |
| | | **Jumla Ndogo** | **25** | **209** | **234** | **229** | **192** | **0** | **5** |
| 3. | Dawa za mitishamba | Mapya | 0 | 22 | 22 | 10 | 8 | 0 | 12 |
| | | Huisha | 0 | 3 | 3 | 1 | 0 | 0 | 2 |
| | | **Jumla Ndogo** | **0** | **25** | **25** | **11** | **8** | **0** | **14** |
| 4. | Vipukusi | Mapya | 0 | 27 | 27 | 24 | 7 | 0 | 3 |
| | | Huisha | 0 | 2 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| | | **Jumla Ndogo** | **0** | **29** | **29** | **26** | **7** | **0** | **3** |
| **Jumla kuu- 1** | | | **342** | **2,044** | **2,390** | **2,193** | **1,328** | **51** | **313** |
| **Jumla kuu – 2** | | | **2** | **13** | **15** | **15** | **8** | **0** | **0** |
| **Jumla kuu 1+2** | | | **344** | **2,057** | **2,405** | **2,208** | **1,336** | **51** | **313** |

*Baki ya maombi 246 ya binadamu inajumuisha maombi 150 ambayo yamefanyiwa tathimini ya kwanza pekee na maombi 96 ambayo yanahitaji kufanyiwa tathmini ya kwanza na pili.

*Kwa mujibu wa **Jedwali Na.1:** maombi 2,208 sawa na 91.6% ya maombi ya usajili wa dawa za binadamu, mifugo, mitishamba na vipukusi yaliyokuwepo yaliyofanyiwa tathmini ambapo maombi 1,336 yaliidhinishwa. Vilevile maombi 51 yalikataliwa usajili wake kutokana na kutokutimiza vigezo vya ubora, usalama na ufanisi.*

## Jumla Maombi ya Usajili



**Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Maombi Mengine Yanayohusu Usajili wa Bidhaa**

| Na | Bidhaa | Maelezo | Baki ya Juni, 2023 | Pokelewa | Jumla | Tathminiwa | Idhinishwa | Kataliwa | Baki |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | **Dawa za Binadamu** | Mabadiliko | 136 | 1368 | 1504 | 1286 | 803 | 0 | 218 |
| | | Hoja | 160 | 1277 | 1437 | 1253 | 0 | 0 | 184 |
| | | **Jumla ndogo** | **296** | **2645** | **2941** | **2539** | **803** | **0** | **402** |
| 2 | **Mifugo** | Mabadiliko | 6 | 37 | 43 | 34 | 7 | 0 | 3 |
| | | Hoja | 18 | 219 | 237 | 209 | 0 | 0 | 10 |
| | | **Jumla ndogo** | **24** | **256** | **280** | **243** | **7** | **0** | **13** |
| 3 | **Mitishamba** | Mabadiliko | 0 | 8 | 8 | 8 | 4 | 0 | 0 |
| | | Hoja | 6 | 13 | 19 | 17 | 0 | 0 | 2 |
| | | **Jumla Ndogo** | **6** | **21** | **27** | **25** | **4** | **0** | **2** |
| 4 | **Vipukusi** | Mabadiliko | 0 | 6 | 6 | 6 | 0 | 0 | 0 |
| | | Hoja | 0 | 18 | 18 | 18 | 2 | 0 | 0 |
| | | **Jumla ndogo** | **0** | **24** | **24** | **24** | **2** | **0** | **0** |
| 5 | **Majaribio ya dawa** | Mabadiliko | 0 | 41 | 41 | 38 | 3 | 0 | 35 |
| | | Hoja | 14 | 21 | 35 | 34 | 27 | 0 | 7 |
| | | **Jumla ndogo** | **14** | **62** | **76** | **72** | **30** | **0** | **42** |
| 6 | **Matangazo ya dawa** | Mapya | 99 | 456 | 555 | 548 | 488 | 0 | 7 |
| | | Hoja | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | | **Jumla** | **99** | **456** | **555** | **548** | **488** | **0** | **7** |
| | **Jumla Kuu** | | **439** | **3,464** | **3,903** | **3,451** | **1,334** | **0** | **466** |

Kwa mujibu wa **Jedwali Na.2:** Maombi mengine 3,451(88.4%) kati ya 3,903 yaliyohusu usajili wa dawa na vipukusi yalifanyiwa tathmini.

### 1.1.9 Tathmini na Usajili wa Majaribio ywa Dawa *(Clinical Trials)*

Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Juni, 2025, Mamlaka ilipokea jumla ya maombi 54 (mapya 13 na mabadiliko 41) ya majaribio ya dawa na chanjo ambapo kati ya maombi mapya 13 yaliyopokelewa, maombi 9 (69.2%) yalikuwa ya majaribio ya dawa, maombi 3 (23.1%) yalikuwa ya bidhaa za kibaiolojia na ombi 1 (7.7%) halitumii dawa, chanjo au kifaa tiba wakati wa kufanya jaribio hilo (non-interventional study). Aidha, kulikuwa na maombi 2 mapya yaliyobaki kwa mwaka wa fedha 2023/24. Hivyo, kufanya jumla ya maombi yaliyokuwepo kwa kipindi hiki kuwa 56. Maombi yote 56 yaliyokuwepo (mapya 15 na mabadiliko 41) yalifanyiwa tathmini.

Maombi yaliyotathminiwa katika kipindi hiki ni pungufu ya maombi matatu (3) ukilinganisha na maombi 59 (mapya 11 na mabadiliko 48) yaliyofanyiwa tathmini katika kipindi kama hiki mwaka 2023/24. Upungufu huu umetokana na idadi ndogo ya maombi iliyopokelewa katika kipindi hiki. Kati ya maombi yaliyotathminiwa, maombi 46 (mapya 8 na mabadiliko 38) yaliidhinishwa na maombi 10 yalikuwa na hoja.

Vilevile, katika kipindi hiki kulikuwa na jumla ya majibu ya hoja (Querry Responses) 35 ambapo majibu 34 kati ya hayo yalifanyiwa kazi na 27 kuidhinishwa. Majibu ya hoja saba (7) hayakukidhi vigezo.

## 1.1.10 Usajili na Utoaji wa Vibali vya Maeneo ya Biashara ya Dawa na Vipukusi.

Mfumo wa usajili wa maeneo ya biashara za bidhaa za dawa na vipukusi husaidia kuhakikisha kuwa maeneo husika yanakidhi vigezo ili kutoathiri usalama, ubora na ufanisi wa bidhaa tajwa. **Jedwali Na. 3** linaonesha mchanganuo wa usajili wa maeneo ya biashara ya dawa na vipukusi.

**Jedwali Na. 3:Maombi ya Usajili wa Maeneo na Utoaji wa Vibali vya Biashara ya Dawa na Vipukusi**

| Aina ya jingo | | | Baki Kutoka 2023 | Yaliyopokelewa | | Jumla | Yaliyotathminiwa | Yaliyosajiliwa | Vibali vilivyotolewa | Kataliwa/Hoja | % yaliyokidhi vigezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mapya | Huisha | | | | | | |
| Dawa | Viwanda vya ndani | | 0 | 2 | 12 | 14 | 14 | 13 | 13 | 1 | 92.9 |
| | Maghala | | 11 | 5 | 63 | 79 | 79 | 78 | 78 | 1 | 98.7 |
| | Duka la jumla la waingizaji dawa (Binadamu) | | 21 | 58 | 91 | 170 | 170 | 152 | 152 | 14 | 89.4 |
| | Duka la jumla la waingizaji dawa (Mifugo) | | 21 | 11 | 75 | 107 | 107 | 105 | 105 | 2 | 98.1 |
| | Maduka ya rejareja (mifugo) | | 7 | 0 | 0 | 7 | 7 | 7 | 7 | 0 | 100 |
| | Duka la dawa muhimu (DLDM) Binadamu | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| | Magari ya kubebea dawa | | 17 | 21 | 50 | 88 | 88 | 88 | 88 | 0 | 100 |
| | **Jumla ndogo** | | **77** | **97** | **291** | **465** | **465** | **443** | **443** | **18** | **95.3** |
| Vipukusi | Viwanda | Vikubwa | 0 | 0 | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 0 | 100 |
| | | Kati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| | | Vidogo | 0 | 0 | 14 | 2 | 14 | 14 | 2 | 0 | 100 |
| | **Jumla ndogo** | | **0** | **0** | **16** | **4** | **4** | **4** | **4** | **0** | **100** |
| **JUMLA KUU** | **Jumla Kuu** | | **77** | **97** | **307** | **469** | **469** | **447** | **447** | **18** | **95.3** |

Kwa mujibu wa **Jedwali Na. 3** kulikuwa na maombi 469 ya usajili wa viwanda na maeneo ya biashara ya dawa na vipukusi ambapo maombi yote yalifanyiwa kazi na maombi 447 sawa na 95% yaliidhinishwa, kusajiliwa na kupewa vibali vya biashara. Maombi yaliyofanyiwa kazi ni pungufu ya maombi 127 (21%) ikilinganishwa na maombi 596 yaliyofanyiwa kazi katika kipindi kama hiki mwaka uliopita. Upungufu huu umetokana na baadhi ya wafanyabiashara kutohuisha leseni za biashara kutokana na kufunga biashara kwa sababu mbali mbali.

# 1.2.0 Ukaguzi wa Maeneo ya Biashara za Dawa na Vipukusi

## 1.2.1 Maeneo ya Biashara za Dawa, Vipukusi na Majaribio ya Dawa

Maeneo ya biashara za dawa na vipukusi hukaguliwa wakati wote ndani ya nchi kwa lengo la kuhakiki ubora wa majengo, usambazaji, uhifadhi na uuzaji ili kudhibiti ubora na usalama wa bidhaa hizo. Maeneo hayo ni pamoja na viwanda vya dawa, maghala ya kuhifadhia dawa, famasi za dawa za binadamu na mifugo, hospitali, vituo vya afya, maghala na magari ya kubeba bidhaa hizi. Mchanganuo wa maeneo yaliyokaguliwa umeainishwa katika **Jedwali Na. 4.**

**Jedwali Na. 4:Ukaguzi wa Viwanda vya Ndani na Maeneo ya Biashara za Dawa na Vipukusi**

| Aina ya Biashara | | | Yaliyopangwa kukaguliwa | Yaliyokaguliwa | | | | Yaliyokidhi vigezo | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Yaliyosajiliwa | Yasiyosajiliwa | Jumla | % | Idadi | % |
| Dawa na Vipukusi | Viwanda | Vikubwa | 18 | 6 | 9 | **15** | 83 | 13 | 87 |
| | | Kati | 4 | 2 | 0 | **2** | 50 | 2 | 100 |
| | | Vidogo | 6 | 15 | 0 | **15** | 250 | 15 | 100 |
| | Maghala ya kuhifadhia dawa | | 47 | 36 | 0 | **36** | 77 | 36 | 100 |
| | Duka la dawa/Famasi - binadamu (Jumla) | | 376 | 394 | 1 | **395** | 105 | 394 | 100 |
| | Duka la dawa/famasi – binadamu (rejareja) | | 1,526 | 1,913 | 41 | **1954** | 128 | 1,913 | 98 |
| | Duka la dawa jumla (famasi) – Mifugo | | 220 | 246 | 1 | **247** | 112 | 238 | 96 |
| | Duka la dawa muhimu (DLDM)- Binadamu | | 5,948 | 4,745 | 1,794 | **6539** | 110 | 4,990 | 76 |
| | Duka la dawa za mifugo | | 877 | 649 | 196 | **845** | 96 | 686 | 81 |
| | Magari ya kubebea dawa | | 18 | 23 | 3 | **26** | 144 | 23 | 88 |
| | "Infusion units" | | 1,405 | 1,063 | 564 | **1627** | 116 | 1,063 | 65 |
| | Hospitali | | 445 | 632 | 3 | **635** | 143 | 625 | 98 |
| | Kliniki | | 209 | 110 | 4 | **114** | 55 | 110 | 96 |
| | Vituo vya afya | | 558 | 622 | 3 | **625** | 112 | 619 | 99 |
| | Zahanati | | 1,365 | 936 | 25 | **961** | 70 | 936 | 97 |
| | Maabara | | 1,028 | 1014 | 6 | **1,020** | 99 | 883 | 86 |
| **JUMLA KUU** | | | **13,599** | **11,935** | **2,640** | **14,593** | **1,185** | **11,086** | **81.6** |

Kwa mujibu wa **Jedwali Na. 4** hapo juu Mamlaka ilifanya kaguzi katika maeneo 14,593 ya biashara za dawa na vipukusi sawa na 107% ya maeneo 13,599 yaliyopangwa.

Maeneo yaliyokaguliwa katika kipindi hiki ni ongezeko la maeneo 1,220 (9%) ikilinganishwa na maeneo 13,373 yaliyokaguliwa mwaka uliopita.

### 1.2.2 Ukaguzi wa Viwanda vya Kutengeneza Dawa Ndani ya Nchi

Kwa mujibu wa Jedwali Na. 4 hapo juu, Mamlaka ilipanga kukagua viwanda vyote 18 vya dawa ndani ya nchi ambapo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2025 jumla ya viwanda 12 sawa na 67% vilikaguliwa. Kati ya viwanda vilivyokaguliwa viwanda nane (8) vilikuwa vya dawa za binadamu na vinne (4) vilikuwa vya dawa za mifugo. Viwanda sita (6) vilivyokuwa katika mpango kazi havikukaguliwa kwa sababu ya kuwa katika matengenezo makubwa.

#### Ukaguzi wa Viwanda vya Kutengeneza Dawa Nje ya Nchi

Jumla ya maombi 172 ya ukaguzi wa viwanda nje ya nchi yalipokelewa katika kipindi cha mwaka 2024/2025. Aidha, kulikuwa na baki ya maombi 502 na hivyo kufanya jumla ya maombi kuwa 674. Kati ya maombi yote yaliyokuwepo, viwanda 110 vilikaguliwa kwa utaratibu wa ana kwa ana na 305 kwa njia ya tathmini ya nyaraka. Idadi hiyo inafanya jumla ya viwanda vilivyokaguliwa kuwa 415 sawa na 218% ya lengo la kukagua viwanda 190 kwa mwaka 2024/25.

### 1.2.3 Ukaguzi Maalum wa Dawa Tiba Zenye Asili ya Kulevya

Kwa kushirikiana na taasisi nyingine za udhibiti za Serikali, Mamlaka ilifanya ukaguzi maalum (operesheni) kwenye maeneo mbalimbali nchini ya kuingiza, kutunza, na kusambaza dawa tiba zenye asili ya kulevya (Narcotics na Psychotropics). Taasisi hizo ni Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Baraza la Famasi (PC), Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) na Bohari ya Dawa (MSD), ukaguzi huo ulifanyika katika mikoa 6 iliyopo katika Kanda tano (5) kati ya nane (8) za TMDA (isipokuwa Kanda ya Magharibi, Kanda ya Kusini na Kanda ya Kati).

Lengo la ukaguzi maalum ilikuwa ni kubaini na kuchukua hatua dhidi ya ukiukwaji wa Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura 219. Katika ukaguzi huo jumla ya maeneo 116 (Famasi 33, Hospitali 42, Vituo vya forodha rasmi 9, mipaka isiyo rasmi 15, vituo vya kutolea dawa ya Methadone (MAT) 4, viwanda 2, duka 1 la dawa za mifugo, na vituo 10 vya kutolea huduma za afya) yalikakuguliwa.

Katika ukaguzi huo, maeneo 53 yalikutwa na makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba Sura 219. Maeneo mawili (2) sawa na 1.7% yalikutwa na bidhaa za Serikali kwenye maeneo binafsi ya huduma za afya, maeneo mawili (2) sawa na 1.7% yalikutwa na kosa la Kutotoa taarifa za upotevu wa dawa tiba zenye asili ya kulevya kwenye Mamlaka husika, maeneo matano (5) sawa na 4.3% yalikutwa na viashiria vya uchepushwaji wa dawa tiba zenye asili ya kulevya, maeneo 10 sawa 8.6% yalikutwa na kosa la utunzaji usiokidhi wa nyaraka, maeneo sita (6) sawa na 5.2% yalikutwa na kosa la kutokidhi vigezo vya usalama, maeneo 11 sawa na 9.4% yalikutwa na bidhaa zilizokwisha muda wa matumizi na maeneo 17 sawa na 17.2% yalikutwa na bidhaa zisizosajiliwa.

Bidhaa za dawa na vifaa tiba zenye thamani ya TZS 19,543,638 zilizokamatwa zilikuwa ni mali ya serikali, huku zikiwa hazijasajiliwa nchini pia zikiwa zimeisha muda wa matumizi.

Pia, Mamlaka ilipokea taarifa 8 (3 kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO) na 5 kutoka ndani ya soko) kuhusu uwepo wa dawa bandia na kukusanya taarifa 6 za uwepo wa dawa duni katika soko. Hakuna dawa bandia zilizotolewa taarifa na WHO (rapid alert) zilizopatikana katika soko.

### 1.2.4 Ukaguzi wa Majaribio ya Dawa

Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Juni, 2025 Mamlaka ilifanya ukaguzi wa majaribio ya dawa na chanjo **23** katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Mbeya na Mwanza. Ukaguzi huo ulibaini mapungufu mbali mbali katika majaribio yote ambapo mapungufu hayo kwa kiasi kikubwa yalihusiana na Maabara na machache yalihusiana na nyaraka ambapo wahusika walielekezwa kufanya marekebisho na kushughulikia mapungufu hayo.

### 1.2.5 Udhibiti wa Uingizaji Nchini na Usafirishaji Nje ya Nchi wa Bidhaa za Dawa

Mamlaka imepokea na kuidhinisha maombi ya uingizwaji wa bidhaa za dawa na malighafi za kutengenezea dawa. Mchanganuo wa maombi ya vibali vya kuingiza bidhaa nchini na kusafirisha bidhaa nje ya nchi umeainishwa kwenye **Jedwali Na. 5**

**Jedwali Na. 5: Maombi ya Vibali vya Kuingiza Bidhaa za Dawa Nchini na Kusafirisha Bidhaa Nje ya Nchi**

| Na | Aina ya bidhaa | Yaliyopokelewa | | Vibali vilivyotolewa | | Vibali vilivyokaguliwa katika vituo vya forodha | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kuingia | Kutoka | Kuingia | Kutoka | Kuingia | Kutoka |
| 1 | Dawa | 5,690 | 171 | 5,392 | 146 | 4411 | 54 |
| 2 | Malighafi – Dawa | 705 | - | 690 | - | 549 | - |
| 3 | Vipukusi | - | - | - | - | 7 | - |
| **Jumla** | | **6,395** | **171** | **6,082** | **146** | **4,967** | **54** |

Kwa mujibu wa **Jedwali Na. 5**, jumla ya maombi 6,228 sawa na 95% ya maombi 6,566 yaliyokuwepo yaliidhinishwa. Idadi ya maombi yaliyoidhinishwa katika kipindi hiki ni ongezeko la maombi 309 ikilinganishwa na maombi 5,919 yaliyoidhinishwa katika mwaka uliopita.

Aidha, jumla ya vibali 5,021 (4,967 vya kuingiza nchini bidhaa za dawa na vibali 54 vya kutoa bidhaa za dawa nje ya nchi) vilikaguliwa katika vituo vya forodha. Vibali viliyokaguliwa katika kipindi hiki ni ongezeko la vibali 505 (11%) ikilinganishwa na vibali 4,516 vilivyotolewa mwaka uliopita. Ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa uingizwaji wa shehena za dawa na idadi ya kaguzi zinazofanyika.

### 1.2.6 Kupokea na Kutathmini Taarifa za Matukio Makubwa ya Kiafya (Serious Adverse Events - SAE) Yanayotokea Katika Majaribio ya Dawa

Katika kipindi cha Julai– Juni, 2025, jumla ya taarifa 962 za maudhi makubwa ya kiafya (Serious Adverse Events) yaliyotokea wakati wa majaribio ya dawa na chanjo zilipokelewa. Taarifa 280 (29%) kati 962 zilitoka katika Majaribio yanayoendelea nchini na taarifa 682 (71%) zilitoka katika nchi nyingine ambako majaribio ya dawa na chanjo zinazojaribiwa nchini yanafanyika pia.

Kati ya taarifa hizo, taarifa 250 (89.3%) zilizotoka katika majaribio yanayoendelea nchini zilifanyiwa tathmini na taarifa 215 (31.5%) kati ya tarifa 682 kutoka nchi nyingine zimefanyiwa tathmini. Taarifa 497 zinaendelea kufanyiwa kazi. Hapakuwa na taarifa inayotilia shaka usalama wa bidhaa (investigational medicinal product) zinazotumika kwenye majaribio ambayo ilihitaji hatua za kiudhibiti kuchukuliwa ili kuwalinda washiriki wa majaribio.

## 1.2.7 Ufuatiliaji wa Usalama wa Dawa na Chanjo

Mamlaka hufanya ufuatiliaji wa usalama wa dawa na chanjo baada ya kuwa zimeruhusiwa kuingia sokoni ili kuhakikisha bidhaa hizo ni salama na hazisababishi madhara makubwa kwa jamii. Katika kipindi hiki cha Julai, 2024 hadi Juni, 2025, Mamlaka ilikusanya taarifa mbalimbali za maudhi yaliyotokana na matumizi ya dawa na chanjo na kuzichakata kama ilivyoelezewa hapa chini: -

### i. Kupokea na Kufanya Tathmini ya Taarifa za Maudhi ya Dawa (Adverse Drug Reactions - ADRS)

Jumla ya taarifa 19,702 za maudhi yaliyohisiwa kusababishwa na matumizi ya dawa (ADRs) zilipokelewa na Mamlaka. Kati ya taarifa hizo, taarifa 7,368 (37.4%) zilihusisha wanaume na taarifa 11,684 (59.3%) zilihusisha wanawake. Taarifa 650 (3.3%) hazikujulikana jinsia. Taarifa zote (100%) ziliingizwa katika mfumo wa Vigiflow.

Idadi ya taarifa za ADRs zilizokusanywa ni sawa na 165.5% ya lengo la kitaifa (11,904) kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) kulingana na idadi ya watu 59,517,754 nchini (Sensa ya Watu na Makazi, 2022).

Taarifa 110 (0.56%) zilihusisha maudhi makubwa (serious adverse drug events) ambapo kati ya hizo, taarifa 58 (52.7%) zimefanyiwa uchunguzi na tathmini.

**Jedwali Na. 6:Taarifa za Madhara Zilizopokelewa Kwa Mwaka Mzima 2024/2025**

| Na | Aina ya tarifa | Pokelewa | Tathminiwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Adverse Drug Reactions - ADRs | 19,702 | 19,702 | Idadi ya taarifa za ADRs zilizokusanywa ni sawa na 165.5% ya lengo la kitaifa (11,904) |
| 2 | Adverse Events Following Immunization – AEFI | 7,017 | 7,017 | Idadi hii ni sawa na 584.8% ya lengo la mwaka (1,200) |

**Jedwali Na. 7:Idadi ya Maudhi ya Dawa Chunguzwa na Tathminiwa kwa Kanda**

| Na | Kanda | Jumla | Chunguzwa | Tathminiwa |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kanda ya Nyanda za Juu Kusini | 21 | 6 | 6 |
| 2. | Kanda ya Mashariki | 24 | 15 | 15 |
| 3. | Kanda ya Kati | 11 | 2 | 2 |
| 4. | Kanda ya Kaskazini | 22 | 11 | 11 |
| 5. | Kanda ya Ziwa Magharibi | 7 | 5 | 5 |
| 6. | Kanda ya Ziwa Mashariki | 15 | 15 | 15 |
| 7. | Kanda ya Magharibi | 10 | 4 | 4 |
| 8. | Kanda ya Kusini | 0 | 0 | 0 |
| | **Jumla** | **110** | **58** | **58** |

Uchunguzi wa taarifa zilizobaki unaendelea.

Idadi na matokeo ya taarifa na uhusiano wa dawa na maudhi makubwa hisiswa (drug event combination relatedness) ni kama ifuatavyo; ***certain (4), probable/likely (13), possible (36), unlikely (2) na unassessable (3)***. Taarifa kwenye kundi la *certain* na *probable/likely* zilitokana na maudhi yanayojulikana kusababishwa na dawa husika, taarifa zenye uhusiano wa *possible* ni zile ambazo hali nyingine ya mgonjwa ilichangia kutokea kwa maudhi hayo, taarifa za uhusiano wa *unlikely* ni maudhi ambayo yalibainika kutokusababishwa na dawa hisiwa na taarifa kwenye kundi la *unassessable* ni ambazo uthibitisho uliokusanywa haukutosheleza kufanya tathmini (taarifa zilikuwa zinakinzana). Hivyo basi, kufuatia tathmini hii hakuna taarifa yoyote iliyohitaji hatua za kiudhibiti kuchukuliwa.

## ii. Kupokea na Kufanya Tathmini ya Taarifa ya Maudhi Yatokanayo na Matumizi ya Chanjo (Adverse Events Following Immunization – AEFI)

Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Juni, 2025, Mamlaka ilipokea jumla ya taarifa 7,017 za maudhi yaliyohisiwa kusababishwa na matumizi ya chanjo (AEFI) ambapo taarifa za wanaume zilikuwa 3,388 (48.3%) na wanawake 3,523 (50.2%). Na taarifa 106 (1.5%) kati ya taarifa zote za AEFI hazikutaja jinsia za waliopata maudhi yaliyohisiwa kusababishwa na matumizi ya chanjo. Mgawanyo wa idadi ya taarifa kwa kila kanda umeambatishwa.

Taarifa 9 (0.13%) zilihusisha maudhi makubwa (Serious AEFIs) ambapo kati ya hizo taarifa 8 (89%) zimefanyiwa uchunguzi. Orodha ya taarifa hizo imeoneshwa hapa chini.

**Jedwali Na. 8: Idadi ya Maudhi ya Chanjo Chunguzwa na Tathminiwa kwa Kanda**

| Na | Kanda | Jumla | Chunguzwa | Tathminiwa |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kanda ya Mashariki | 1 | 1 | 1 |
| 2. | Kanda ya Kaskazini | 1 | 1 | 1 |
| 3. | Kanda ya Ziwa Magharibi | 3 | 3 | 3 |
| 4. | Kanda ya Magharibi | 3 | 3 | 3 |
| 5. | Kanda ya Nyanda za Juu Kusini | 1 | 0 | 0 |
| | **Jumla** | **9** | **8** | **8** |

Baada ya tathmini idadi ya taarifa na uhusiano wa chanjo na maudhi makubwa hisiwa (vaccine event combination relatedness) ulibainika kama ifuatavyo; vaccine product related (4), indeterminate (2) na coincidental (2).

## iii. Hali ya Ukusanyaji wa Taarifa za Maudhi kwa Kanda

Taarifa 19,702 za maudhi ya dawa zilizokusanywa ni sawa na 165.5% ya lengo la mwaka (11,904) na taarifa 7,017 za maudhi ya chanjo zilizokusanywa ni sawa na 584.8% ya lengo la mwaka (1,200). Aidha, Kanda 4 (50%) zilifikia lengo la mwaka kwa ukusanyaji wa taarifa za maudhi ya dawa na Kanda 6 (75%) zilifikia lengo la mwaka kwa ukusanyaji wa taarifa za maudhi ya chanjo **(Jedwali Na.: 9).**

**Jedwali Na. 9: Idadi Ya Maudhi Kusanywa Kwa Kila Kanda**

| Na | Kanda | Taarifa za Maudhi ya Dawa | | | | Taarifa za Maudhi ya Chajo | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Idadi ya Watu | Lengo (mwaka) | Kusanywa | Mafanikio (%) | Lengo (mwaka) | Kusanywa | Mafanikio (%) |
| 1 | Kanda ya Mashariki | 9,608,486 | 1,922 | 9,148 | 474.3 | 194 | 1,165 | 601.4 |
| 2 | Kanda ya Kati | 8,693,320 | 1,739 | 3,042 | 175 | 175 | 833 | 475.3 |
| 3 | Kanda ya Nyanda za Juu Kusini | 5,928,635 | 1,186 | 2,942 | 248.1 | 120 | 85 | 71.1 |
| 4 | Kanda ya Ziwa Mashariki | 9,276,538 | 1,855 | 2,106 | 113.5 | 187 | 506 | 270.5 |
| 5 | Kanda ya Magharibi | 7,180,488 | 1,436 | 1,135 | 79 | 145 | 143 | 98.8 |
| 6 | Kanda ya Kaskazini | 6,255,374 | 1,251 | 718 | 60.1 | 126 | 581 | 460.7 |
| 7 | Kanda ya Ziwa Magharibi | 8,233,055 | 1,647 | 388 | 23.6 | 166 | 221 | 133.1 |
| 8 | Kanda ya Kusini | 4,341,858 | 868 | 223 | 25.7 | 88 | 3,483 | 3978.7 |
| | **Jumla** | **59,517,754** | **11,904** | **19,702** | **165.5** | **1,200** | **7,017** | **584.8** |

## iv. Hali ya Utoaji wa Taarifa za Maudhi kwa Hospitali na Halmashauri

Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Juni, 2025, taarifa za maudhi ya dawa 16,903 (85.8%) kati ya taarifa zote 19,702 zilitoka katika katika Halmashauri 10 nchini na taarifa za maudhi ya chanjo 4,748 (74.1%) kati ya taarifa zote 7,017 zilitoka katika Halmashauri 10 nchini **(Jedwali Na.: 10)**

**Jedwali Na. 10: Hospitali na Halamashauri Zilizofanya Vizuri Katika Utoaji wa Taarifa**

| Na | Taarifa za ADRs | | Taarifa za AEFI | |
|---|---|---|---|---|
| | **Hospitali** | **Idadi ya ADRs** | **Halmashauri** | **Idadi ya AEFIs** |
| 1 | Ilala CC | 7,687 | Nachingwea DC | 1450 |
| 2 | Dodoma CC | 2,806 | Ilala CC | 997 |
| 3 | Mbeya City | 1,819 | Ruangwa DC | 597 |
| 4 | Ubungo MC | 1,398 | Lindi MC | 482 |
| 5 | Nyamagana MC | 1,040 | Kilwa DC | 415 |
| 6 | Tabora MC | 979 | Nyamagana MC | 349 |
| 7 | Tunduma TC | 439 | Babati DC | 314 |
| 8 | Chato DC | 279 | Dodoma CC | 252 |
| 9 | Mbozi DC, | 250 | Bahi DC | 218 |
| 10 | Arusha CC | 206 | Mtama DC | 201 |
| | **Jumla** | **16,903** | | **5,275** |

### (a) Kupokea na Kutathmini Taarifa za Periodic Safety Update Report (PSUR) na Risk Management Plans (Rmps) za Dawa na Chanjo

Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Juni, 2025, jumla ya taarifa 97 za PSUR na 13 za RMP zilipokelewa Taarifa 57 (58.7%) za PSUR na 7 (53.8%) za RMP zilifanyiwa tathmini na kubainika kutokuwa na changamoto za kiusalama (major safety concerns) zinazohitaji kuchukuliwa hatua za kiudhibiti. Taarifa zilizobaki zitafanyiwa tathmini kipindi kijacho **(Jedwali Na.:11).**

**Jedwali Na. 11: Mchanganuo wa Taarifa za Ufuatiliaji wa Usalama wa Dawa**

| Na | Aina ya taarifa | Pokelewa | Tathminiwa | Hatua |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Adverse Drug Reactions (ADR) | 19,702 | 19,218 | Taarifa 484 zilizobaki zinakosa baadhi ya taarifa muhimu kuwezesha tathmini kufanyika na zinaendelea kurekebishwa. |
| 2 | Adverse Events Following Immunization (AEFI) | 7,017 | 6,732 | Taarifa 285 zilizobaki zinakosa baadhi ya taarifa muhimu kuwezesha tathmini kufanyika na zinaendelea kurekebishwa. |
| 3 | Periodic Safety Update report (PSUR) | 97 | 57 | Kati ya taarifa 54 zilizofanyiwa tathmini hakuna taarifa iliyohitaji kuchukuliwa hatua za kiudhibiti. Taarifa 40 zilizobaki zitafanyiwa tathmini mwaka wa fedha 2025/26. |
| 4 | Risk Management Plan (RMP) | 13 | 7 | Taarifa ilifanyiwa tathmini, hakukua na taarifa ya hofu ya kiusalama iliyohitaji kuchukukuliwa hatua za kiudhibiti. Taarifa 6 zilizobaki zitafanyiwa tathmini mwaka wa fedha 2025/26. |

## (b) Kufanya Vikao vya Kamati ya Usalama wa Dawa na Chanjo (VTC)

Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Juni, 2025, Mamlaka ilifanya vikao 2 (Kikao cha 21 na cha 22) vya Kamati ya Usalama wa Dawa na Chanjo (VTC). Vikao tajwa vilipitia agenda mbalimbali zilizowasilishwa zilizohusu Usalama wa dawa na chanjo na kushauri mambo yafuatayo: -

- Mamlaka iwasiliane na TAMISEMI ili kazi ya ufuatiliaji wa taarifa za maudhi ya Dawa na Chanjo ziingizwe kwenye maelezo ya kazi (Job Description) za Wafamasia
- Mpango wa Taifa wa kudhibiti Malaria (NMCP) wuaingize pia ufuatiliaji wa usalama wa dawa katika supportive supervisión checklist yao na ikiwezekana katika module yao kwenye Afya SS.
- Mamlaka iangalie namna ya kuwa na makubaliano (Memorándum of understanding) na Hospitali kubwa nchini juu ya Ufuatiliaji wa taarifa za maudhi ya dawa na chanjo katika vituo hivyo.
- Mamlaka ipanue wigo wa kuwa na Memorándum of Understanding (MoU) na Hospitali zingine husasani za Kanda.
- Kamati za uchunguzi zilizoteuliwa ziwezeshwe pale inapowezekana ili kuhakikisha uchunguzi unafanyika kwa wakati na taarifa kuwasilishwa.
- Mamlaka iongeze nguvu ya uhamasishaji katika Mikoa ya Pwani, Mtwara, Shinyanga, Morogoro, Songwe, Rukwa, Ruvuma, Katavi na Kigoma ambayo haikuwasilisha kabisa tarifa yoyote.

Mapendekezo ya Kamati (VTC) yameanza kutekelezwa ambapo tayari NMCP wameingiza suala la ufuatiliaji wa usalama wa dawa katika supportive supervisión checklist yao, kupitia ofisi za TMDA Kanda, uhamasishaji umefanyika katika Mikoa ya Pwani, Mtwara, Shinyanga, Ruvuma, Katavi na Kigoma ambayo haikuwasilisha kabisa taarifa yoyote. Makubaliano kati ya Mamlaka na Hospitali kubwa yameanza na yako hatua za mwisho kwa ofisi ya Kanda ya Ziwa Mashariki na Hospitali ya Rufaa ya Bugando.

## (c) Kufanya Mafunzo kwa Wasimamizi wa Pharmacovigilance Kutoka kwa Wamiliki wa Bidhaa (Marketing Authorization Holders) Nchini

Mamlaka kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili (MUHAS) ilifanya mafunzo ya kanuni bora za Ufuatiliaji wa Usalama wa Dawa na Chanjo (Good Pharmacovigilance Practices) kwa wasimamizi 45 wa shughuli za pharmacovigilance (Qualified Focal Person for Pharmacovigilance) pamoja na watumishi wa kada za afya zingine kutoka kwa wasajili na watengenezaji wa dawa nchini. Mchanganuo wa waliopatiwa mafunzo kwa taaluma zao ni kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.:12.**

**Jedwali Na. 12: Washiriki Waliopatiwa Mafunzo ya Pharmacovigilance**

| Na. | Taaluma | Idadi | (%) |
|---|---|---|---|
| 1 | Wafamasia | 27 | 60.0 |
| 2 | Wateknolojia Dawa | 10 | 22.2 |
| 3 | Madaktari | 2 | 4.4 |
| 4 | Mkutubi | 1 | 2.2 |
| 5 | Biomedical Engineer | 1 | 2.2 |
| 6 | Mfamasia Mtarajali | 1 | 2.2 |
| 7 | Wanafunzi wa Famasi | 3 | 6.7 |
| | **Jumla** | **45** | **100** |

### (d) Kufanya Mafunzo na Uhamasishaji wa Utoaji wa Taarifa za Maudhi ya Dawa na Chanjo Nchini

Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Juni, 2025, Mamlaka ilifanya mafunzo ya ufuatiliaji wa usalama wa chanjo kwa kutumia application (app) ya VIGIMOBILE yalitolewa kwa wasimamizi na watoa huduma wa Afya ngazi ya Mkoa na Halmashauri wakiwemo wachanjaji (Vaccinators) kutoka vituo vyote vinavyotoa chanjo katika Mikoa minne (4) ya Lindi, Singida, Mtwara na Iringa ili kuwajengea uwezo wa kutumia App hiyo katika kutoa taarifa za maudhi ya chanjo ambapo jumla ya washiriki 1,279 (RHMT 17, CHMT 105 na Wachanjaji (1,157) walipata mafunzo hayo. **Jedwali Na. 13.**

**Jedwali Na. 13: Idadi ya Waliopatiwa Mafunzo kwa Makundi**

| Kundi | Lindi | Singida | Mtwara | Iringa | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| RHMT | 4 | 5 | 4 | 4 | 17 |
| CHMT | 22 | 28 | 35 | 20 | 105 |
| Wachanjaji | 312 | 279 | 259 | 307 | 1,157 |
| **Jumla** | **338** | **312** | **298** | **331** | **1,279** |

Aidha, wachanjaji 1,157 waliopatiwa mafunzo walikuwa wa kada mbalimbali wengi wao wakiwa Wauguzi (69.4%) wakifuatiwa na Wahudumu wa Afya 16% **(Jedwali Na. 14).**

**Jedwali Na. 14: Taaluma za Wachanjaji Waliopatiwa Mafunzo**

| Taaluma | Lindi | Singida | Mtwara | Iringa | Jumla | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Wauguzi | 211 | 225 | 146 | 221 | 803 | 69.4 |
| Madaktari | 31 | 20 | 41 | 36 | 128 | 11 |
| Wafamasia | 3 | 4 | 6 | 3 | 16 | 1.4 |
| Afisa Afya | 5 | 4 | 9 | 7 | 25 | 2.2 |
| Wahudumu wa Afya | 62 | 26 | 57 | 40 | 185 | 16 |
| **Jumla** | **312** | **279** | **259** | **307** | **1157** | **100** |

## 1.2.8 Ufuatiliaji wa Ubora wa Dawa na Chanjo katika Soko *(Post Marketing Surveilance - PMS)*

Mamlaka hufanya ufuatiliaji wa ubora wa dawa na chanjo baada ya kuwa zimeruhusiwa kuingia sokoni (Post Marketing Surveillance – PMS) ili kuhakikisha bidhaa hizo zinaendelea kuwa na ubora unaotakiwa kwa matumizi ya wananchi. Katika kipindi hiki cha Julai, 2024 – Juni, 2025, Mamlaka ilitekeleza kazi mbali mbali za PMS kama ifuatavyo: -

### (a) Kuandaa Mpango Mpya Wa PMS wa Miaka 3 (2024 – 2027)

Mamlaka iliandaa mpango mpya wa miaka mitatu (3) wa ufuatiliaji wa ubora wa dawa katika soko (PMS) wa 2024 -2027 ambao umeainisha dawa mbalimbali zitakazofuatiliwa katika soko kwa kipindi husika.

### (b) Kutoa mafunzo kwa Wakusanyaji Sampuli

Katika kutekeleza Mpango huo mpya, Mamlaka ilifanyika mafunzo kwa wakaguzi ambao watashiriki katika zoezi la uchukuaji wa sampuli za dawa na chanjo kwa awamu ya kwanza na ya pili ya mpango huo ambapo jumla ya wakusanya sampuli *(sample collectors)* **13** kutoka kanda zote walipatiwa mafunzo hayo ambayo yalilenga kuwajengea uwezo wa namna sahihi ya ukusanyaji wa sampuli kupitia Mpango mpya ulioandaliwa.

Katika mafunzo hayo ilipendekezwa kufanya maboresho katika mfumo wa RIMS ili kuwezesha mabadiliko (variations) ya dawa inaonwa na kila mkaguzi. Ilishauriwa MMRE aweze kuhakikisha dawa zote zilizopewa idhini ya mabadiliko (Variations) zinaingia kwenye mfumo.

## 1.2.9 Utekelezaji wa Kazi za Miradi inayofadhiliwa na Wahisani Mbalimbali

### (a) Utekelezaji wa Mradi wa AU-3S

Mamlaka kuanzia tarehe 1 Septemba, 2024 ilianza kutekeleza Mradi wa *African Union - Smart Safety Surveillance (AU-3S)* unaosimamiwa na AUDA - NEPAD chini ya ufadhili wa *Bill and Melinda Gates (BMGF)*. Mradi huu ni wa miaka miwili (2) na una lengo la kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji wa dawa na chanjo katika nchi za Afrika ikiwa ni pamoja na kutengeneza Kanzidata ya kukusanya pamoja taarifa za maudhi ya dawa na chanjo. Katika kipindi cha Julai, 2024 – Juni, 2025, Mamlaka ilitekeleza kazi tisa (9) kati ya 10 zilizopangwa kama ifuatavyo:

#### i. Mafunzo ya Utoaji wa Taarifa za Maudhi ya Dawa na Chanjo

Mamlaka ilitoa mafunzo na uhamasishaji wa utoaji wa taarifa za maudhi ya dawa na chanjo kwa watoa huduma za afya **52** kutoka Hospitali **13** za Wilaya katika Mikoa 8 nchini. Mafunzo haya yalitolewa kwa Hospitali kutoka Wilaya ambazo zilikuwa na utoaji hafifu wa taarifa hizo. Mchanganuo wa Mikoa, Halmashauri na idadi ya washiriki umeanishwa kwenye **Jedwali Na. 15.**

**Jedwali Na. 15.: Idadi ya Washiriki katika Mikoa na Halmshauri**

| S/N | Mkoa | Halmashauri | Wafamasia | Madaktari | Wauguzi | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Singida | Ikungi DC | 2 | 1 | 1 | 4 |
| | | Iramba DC | 2 | 1 | 1 | 4 |
| 2 | Manyara | Babati DC | 2 | 1 | 1 | 4 |
| | | Kiteto DC | 2 | 1 | 1 | 4 |
| 3 | Ruvuma | Songea DC | 2 | 1 | 1 | 4 |
| 4 | Mara | Butiama DC | 2 | 1 | 1 | 4 |
| 5 | Tabora | Nzega DC | 2 | 1 | 1 | 4 |
| | | Igunga DC | 2 | 1 | 1 | 4 |
| 6 | Mbeya | Busokelo DC | 2 | 1 | 1 | 4 |
| | | Mbarali DC | 2 | 1 | 1 | 4 |
| 7 | Shinyanga | Msalala DC | 2 | 1 | 1 | 4 |
| 8 | Tanga | Handeni DC | 2 | 1 | 1 | 4 |
| | | Mkinga DC | 2 | 1 | 1 | 4 |
| | **Jumla** | | **26** | **13** | **13** | **52** |

#### ii. Kuboresha Mfumo wa Mamlaka wa Kutolea na Kuchakata Taarifa za Maudhi ya Dawa na Chanjo (Safety and Quality Reporting Tool – SQRT)

Mfumo wa Kielektroniki wa Mamlaka unaoitwa Safety and Quality Reporting Tool (SQRT) ulifanyiwa maboresho (upgraded) kwa kurekebisha na kuongeza maeneo yote muhimu ya kuingiza taarifa za maudhi. Maboresho yaliyofanyika ni pamoja na;



Mfumo kuweza kuonyesha kama taarifa zilizopokelewa kupitia USSD (*152*00#) kama zimefanyiwa kazi na Mamlaka kwa kupigiwa simu au hazijafanyiwa kazi (new, nullified and accepted status).

Mifumo ya kutolea taarifa ya SQRT App na SQRT Web kuwekewa vipengele vyote vinavyopatikana kwenye Fomu za Mamlaka za kutolea taarifa za maudhi ya dawa na chanjo. Vipengele hivyo vinajumuisha taarifa za mgonjwa, dawa, maudhi aliyopata na taarifa za mtoaji taarifa.

Mfumo kuweza kutoa takwimu za maudhi ya dawa na chanjo kwa kuzingatia aina ya bidhaa, sehemu taarifa ilikotoka (Kanda, Mikoa, Halmashauri), aina ya maudhi n.k.

Mfumo kuweza kutoa michoro pamoja na majedwali ya takwimu (graphical data presentation and summary tables) ya taarifa za maudhi ya dawa na chanjo.

Mfumo kuweza kuchuja taarifa kadri mtumiaji anavyohitaji mfano taarifa zilizopokelewa katika kipindi cha mwezi, robo mwaka au nusu mwaka.

Mfumo kuweza kutoa dondoo (extract) za taarifa za maudhi ya dawa na chanjo katika umbizo ya ekseli (Excel Fomart)

**iii. Uhamasishaji wa Utoaji wa Taarifa za Maudhi Yatokanayo na Matumizi ya Chanjo na Dawa kwa Jamii (Community Sensitization)**

Mamlaka ilifanya uhamasishaji wa utoaji wa tarifa za maudhi ya dawa na chanjo kwa wananchi (jamii) katika halmashauri saba (7) nchini ambazo zilikuwa na viwango vya chini vya utoaji taarifa za maudhi ya dawa na chanjo ambapo jumla ya wananchi 13,643 (Wanaume 5,649 na wanawake 7,994) walifikiwa na kuhamasishwa (Jedwali **Na.:16)**.

**Jedwali Na. 16: Idadi ya Waliohamasishwa kwa Kila Halmashauri**

| Na | Mkoa | Halmashauri | Idadi ya Waliohamasishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| 1 | Geita | Geita DC | 121 | 302 | 423 |
| 2 | Iringa | Mafinga DC | 702 | 1,887 | 2,589 |
| 3 | Tabora | Nzega DC | 205 | 360 | 565 |
| 4 | Tanga | Tanga CC | 728 | 1,230 | 1,958 |
| 5 | Simiyu | Bariadi TC | 3,459 | 3,397 | 6,856 |
| 6 | Njombe | Makambako TC | 186 | 480 | 666 |
| 7 | Arusha | Monduli DC | 248 | 338 | 586 |
| | **Jumla** | | **5,649** | **7,994** | **13,643** |

**iv. Kutengeneza Mahitaji ya Kuunganisha Mfumo wa SQRT na Mfumo wa *Afrivigilance Hub wa African Union (AU)***

Mahitaji ya kuunganisha mfumo wa SQRT na Mfumo Mpya wa kukusanya taarifa za maudhi ya dawa na chanjo Afrika *(Afrivigilance)* yalitengenezwa kwa kupitia Mwongozo uliotolewa na AUDA-NEPAD ambapo *Active Programming Interface (API)* ilitengenezwa.

v. **Kuunganishwa kwa Mfumo wa SQRT na Mfumo wa Afrivigilance Hub**

Mfumo wa SQRT ulioboreshwa uliunganishwa na Mfumo wa Afrivigilance Hub kwa ajili ya kuwasilisha taarifa za maudhi ya dawa na chanjo kwenye Mfumo huo. Hii itasaidia kubadilishana taarifa za bara la Afrika ili kusaidia maamuzi ya udhibiti wa usalama wa dawa na chanjo.

vi. **Mafunzo ya Mfumo wa Safety and Quality Reporting Tool (SQRT) Ulioboreshwa**

Kufuatia Mfumo wa SQRT kuboreshwa, Mamlaka ilifanya mafunzo kwa waratibu 15 wa shughuli za pharmacovigilance kutoka Kanda na Makao makuu ili kuwajengea uwezo wa namna ya kupokea, kushughulikia na kuchakata taarifa wanazozipokea kwenye mfumo huo.

vii. **Kuandaa Mwongozo wa Kutambua na Kushugulikia Maudhi Mapya ya Dawa Na Chanjo (Guidelines For Signal Detection and Management)**

Mamlaka iliandaa Mwongozo wa kutambua na kushughulikia maudhi mapya ya dawa na chanjo (Guidelines for Signal Detection and Management). Mwongozo huu umezingatia namna ya kubaini maudhi hayo, kuyathibitisha na kutumiwa na Mamlaka katika kufanya maamuzi juu ya usalama wa dawa na chanjo.

viii. **Kununua na Kusambaza Kompyuta katika Vituo vya Ufuatiliaji wa Usalama wa Dawa na Chanjo**

Mamlaka ilinunua na kusambaza kompyuta tano (5) katika Vituo vitano (5) vya Ufuatiliaji wa Usalama wa dawa na chanjo vya ngazi ya Mikoa (Regional Pharmacovgilance centres) ili kusaidia uingizwaji wa haraka wa taarifa za maudhi ya dawa na chanjo katika Kanzidata ya VIGIFLOW na kusaidia uchakataji wa taarifa hizo kwa wakati na kuchukua hatua haraka pale inapobidi. Mchanganuo wa Vituo hivyo ni kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.:17**

**Jedwali Na. 17: Orodha ya Hospitali Zilizopelekewa Kompyuta**

| Na. | Jina la Kituo | Mkoa | Kanda |
|---|---|---|---|
| 1 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu | Simiyu | Kanda ya Ziwa Mashariki |
| 2 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma Maweni | Kigoma | Kanda ya Magharibi |
| 3 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe | Songwe | Kanda ya Nyanda za Juu Kusini |
| 4 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma | Dodoma | Kanda ya Kati |
| 5 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa | Iringa | Kanda ya Kati |

ix. **Mafunzo ya Pharmacovigilance kwa Waratibu wa Mipango Misonge *(Public Health Programs)***

Mamlaka ilifanya mafunzo ya *pharmacovigilance* kwa Waratibu wa Mipango Misonge kutoka ngazi ya Taifa na Mikoa nane (8) nchini ambayo ni Mtwara, Katavi, Simiyu, Iringa, Shinyanga, Tanga, Rukwa na Manyara. Jumla ya Waratibu 36 (4 kutoka ngazi ya taifa na 32 kutoka ngazi ya Mikoa) walipatiwa mafunzo hayo ili kuwajengea uwezo kwenye ufuatiliaji na utoaji wa taarifa za maudhi yanayotokana na bidhaa (dawa na chanjo) zinazotumiwa kwenye Mipango Misonge. Waratibu kutoka Mipango ifuatayo walishirikishwa:

- Mpango wa Kudhibiti UKIMWI, Magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini (NaSHCoP);
- Mpango wa Taifa wa Kifua Kikuu na Ukoma (NTLP);
- Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Magonjwa yaliyokuwa hayapewi Kipaumbele (NTD); na
- Mpango wa Afya wa Chanjo (IVD)

### (b) Utekelezaji wa Kazi za Mradi wa Saving Lives and Livelihood Chini ya AKROS Research Initiative)

Kuanzia mwezi Februari, 2025 Mamlaka ilianza kutekeleza Mradi unaoitwa Saving Lives and Livelihood (SLL) chini ya Usimamizi wa AKROS *Research Initiative* kwa ufadhili wa African CDC na *Mastercard Foundation*. Mradi huu wa miezi 10 utakamilika Disemba, 2025.Lengo kuu la mradi ni kuimarisha idadi na ubora wa taarifa za maudhi ya dawa na chanjo. Kufikia mwezi Juni, 2025, Mamlaka imetekeleza kazi 3 kama ifuatavyo;

**i. Mafunzo ya Tathmini (Causality Assessment) ya Taarifa za Maudhi ya Dawa na Chanjo**

Mafunzo ya tathmini (causality assessment) ya taarifa za maudhi ya dawa na chanjo yalifanyika kwa Waratibu wa pharmacovigilance 13 kutoka Ofisi za Kanda na Makao Makuu na kwa wajumbe tisa (9) wa Kamati Mpya ya Usalama wa Dawa (Vigilance Technical Committee).

**ii. Mafunzo ya Pharmacovigilance kwa Watoa Huduma za Afya Katika Mkoa wa Mwanza**

Mafunzo ya utoaji wa taarifa za maudhi ya dawa na chanjo yalifanyika katika Halmashauri nane (8) na Vituo vya kutolea huduma za afya 80 ambapo jumla ya watoa huduma za afya 708 walipatiwa mafunzo kama ifuatavyo;

**Aina ya Vituo vya Kutolea Huduma za Afya Vilivyopatiwa Mafunzo**

Mafunzo yalitolewa kwa jumla ya vituo vya kutolea huduma za afya 80 (Hospitali 10, Vituo vya Afya 43 na Zahanati 27) **(Jedwali Na.: 18)**

**Idadi ya vituo vilivyopatiwa mafunzo**

80 Mafunzo yalitolewa

10 Hospitali

43 Vituo vya afya

27 Zahanati

**Jedwali Na. 18: Idadi na aina ya Vituo vya Huduma kwa Halmashauri Mkoa wa Mwanza vilivyopatiwa mafunzo**

| Na. | Aina ya Kituo | Ilemela DC | Nyamagana DC | Misungwi DC | Ukerewe DC | Magu DC | Kwimba DC | Sengerema DC | Buchosa DC | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Hospitali | 02 | 01 | 01 | 01 | 01 | 01 | 02 | 01 | **10** |
| 2. | Vituo vya Afya | 05 | 02 | 07 | 06 | 07 | 09 | 05 | 01 | **43** |
| 3. | Zahanati | 03 | 07 | 02 | 03 | 02 | 0 | 03 | 08 | **27** |
| | **Jumla** | **10** | **10** | **10** | **10** | **10** | **10** | **10** | **10** | **80** |

## Idadi ya Waliofundishwa kwa Kila Kada na Halmashauri

Jumla ya Watoa Huduma za Afya **708** (wanaume 306 na wanawake 402) walipatiwa mafunzo kutoka kwenye Halmashauri zote nane (8) za Mkoa wa Mwanza. Wengi walikuwa wauguzi 307 (43.3%) wakifuatiwa na tabibu 164 (23.2%) **(Jedwali Na. 19).**

**Jedwali Na. 19: Idadi ya Waliofundishwa kwa Kada na Halmashauri Mkoa wa Mwanza**

| Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya Waliofundishwa (Kwa Kada) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Tabibu | Famasi | Wauguzi | Maabara | *Wengine | Jumla |
| 1 | Ilemela MC | 30 | 15 | 40 | 8 | 7 | **100** |
| 2 | Sengerema DC | 26 | 9 | 48 | 2 | 11 | **96** |
| 3 | Magu DC | 23 | 6 | 54 | 4 | 2 | **89** |
| 4 | Kwimba DC | 17 | 7 | 30 | 9 | 19 | **82** |
| 5 | Misungwi DC | 30 | 16 | 42 | 10 | 0 | **98** |
| 6 | Buchosa DC | 3 | 9 | 20 | 3 | 42 | **77** |
| 7 | Ukerewe DC | 13 | 18 | 36 | 10 | 6 | **83** |
| 8 | Nyamagana MC | 22 | 14 | 37 | 5 | 5 | **83** |
| | **Jumla** | **164** | **94** | **307** | **51** | **92** | **708** |

*Wahudumu wa Afya, Afisa Afya

**iii. Mafunzo ya Pharmacovigilance kwa Watoa Huduma za Afya katika Mkoa wa Geita.**

Mafunzo ya utoaji wa taarifa za maudhi ya dawa na chanjo yalifanyika katika Halmashauri zote 6 za Mkoa wa Geita. Jumla ya watoa huduma 541 toka vituo vya kutolea huduma za afya 60 walipatiwa mafunzo husika.

## Aina ya Vituo vya Kutolea Huduma za Afya Vilivyopatiwa Mafunzo

Mafunzo yalitolewa kwa jumla ya vituo vya kutolea huduma za afya 60 (Hospitali 7, Vituo vya Afya 33 na Zahanati 20) *(Jedwali Na.: 20)*

**Jedwali Na. 20: Idadi na Aina ya Vituo vya Huduma kwa Halmashauri Mkoa wa Geita vilivyopatiwa mafunzo**

| Na. | Aina | Bukombe DC | Chato DC | Geita DC | Geita MC | Mbogwe DC | Nyang'hwale DC | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Hospitali | 01 | 01 | 02 | 01 | 01 | 01 | **07** |
| 2. | Vituo vya Afya | 05 | 09 | 07 | 04 | 04 | 04 | **33** |
| 3. | Zahanati | 04 | 0 | 01 | 05 | 05 | 05 | **20** |
| | **Jumla** | **10** | **10** | **10** | **10** | **10** | **10** | **60** |



## Idadi ya Waliofundishwa kwa Kila Kada na Halmashauri

Jumla ya Watoa Huduma za Afya 541 walipatiwa mafunzo kutoka kwenye Halmashauri zote sita (6) za Mkoa wa Geita. Wengi walikuwa Wauguzi 202 (37.3%) wakifuatiwa na Tabibu 149 (27.5%) **(Jedwali Na.:21).**

**Jedwali Na. 21: Idadi ya Waliofundishwa kwa Kada na Halmashauri Mkoa wa Geita**

| Na. | Jina la Halmashauri | Idadi ya Waliofundishwa (Kwa Kada) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Tabibu | Famasi | Wauguzi | Maabara | *Wengine | Jumla |
| 1 | Bukombe DC | 22 | 10 | 23 | 08 | 17 | **80** |
| 2 | Chato DC | 33 | 09 | 36 | 12 | 10 | **100** |
| 3 | Geita DC | 24 | 10 | 36 | 12 | 08 | **90** |
| 4 | Mbogwe DC | 24 | 11 | 44 | 11 | 11 | **101** |
| 5 | Geita DC | 24 | 07 | 35 | 08 | 05 | **79** |
| 6 | Nyang'hwale DC | 22 | 12 | 28 | 13 | 16 | **91** |
| | **Jumla** | **149** | **59** | **202** | **64** | **67** | **541** |

*Wahudumu wa Afya, Afisa Afya

## (c) Utekeleza wa Mradi wa BREEDIME

Mamlaka tangu tarehe 1 Juni, 2023 imekuwa ikitekeleza Mradi wa miaka mitatu (3) unaoitwa *"Building resilient research ethics, Diagnostics and medicines regulatory capacity during routine and public health emergency periods"* kwa ufupi "BREEDIME" wenye lengo la kuimarisha udhibiti wa majaribio na ufuatiliaji wa ubora wa dawa, chanjo na vifaa tiba.

Mradi huo unatekelezwa kwa kushirikiana na taasisi nyingine 7 ambazo ni; Muhimbili University of Health and Allied Sciences (MUHAS), Kilimanjaro Christian Research Institute (KCRI), Rwanda Food and Drugs Authority (Rwanda FDA), Karolinska Institute (KI), Sweden; Zanzibar Food and Drug Agency (ZFDA), Zanzibar Health Research Institute (ZAHRI); National Institute for Medical Research (NIMR), na University of St. Andrew, United Kingdom. Katika kipindi cha kuanzia tarehe 1 Julai, 2024 hadi Juni, 2025, kazi zifuatazo za Mradi wa BREEDIME zimetekelezwa;

### i. Ukusanyaji wa Sampuli, Tathmini ya Lebo na Uchunguzi wa Maabara

Kupitia Mradi wa BREEDIME, kazi ya kufuatilia ubora wa dawa sokoni (PMS) ilifanyika ambapo jumla ya sampuli 210 za dawa aina ya *Amoxicillin, Azithromycin na cotrimoxazole* (vidonge na maji) zilikusanywa na tathimini ya taarifa za dawa hizo kwenye karatasi zake *(product information review)* ilifanyika.

Jumla ya sampuli 105 (50%) kati ya 210 zilizokusanywa hazikukidhi vigezo na masharti ya labelling na hivyo hatua za kiudhibiti zilichukuliwa ikiwa ni pamoja na wasajili wa dawa hizo kutakiwa kubadilisha lebo kwa kuongeza taarifa zilizokuwa zinakosekana. Mchanganuo wa makundi na matokeo ya tathmini ya taarifa za sampuli hizo za dawa umeainishwa katika **Jedwali Na.:22.**

Jedwali Na. 22: Mchanganuo wa Matokeo ya Tathmini za Lebo za Sampuli za Dawa

| Muundo na Aina ya Dawa | Idadi ya Sampuli | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Dawa zilizoingizwa nchini | | | Dawa zilizotengenezwa nchini | | |
| | Kusanywa | Faulu | Shindwa | Kusanywa | Faulu | Shindwa |
| *Azithromycin 250mg Tablets* | 12 | 1 | 11 | 5 | 4 | 1 |
| *Azithromycin 500mg Tablets* | 19 | 17 | 2 | 8 | 7 | 1 |
| *Azithromycin Oral Suspension* | 33 | 16 | 17 | 0 | 0 | 0 |
| *Amoxicillin 250mg Capsules* | 39 | 37 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| *Amoxicillin 500mg Capsules* | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| *Amoxicillin Pediatric Oral Suspension* | 25 | 0 | 25 | 0 | 0 | 0 |
| *Co-trimoxazole 480mg and 960mg tablets* | 26 | 17 | 9 | 8 | 0 | 8 |
| *Co-trimoxazole Oral Suspension* | 17 | 3 | 14 | 16 | 1 | 15 |
| **Jumla** | **173** | **93** | **80** | **37** | **12** | **25** |

NB: Uchunguzi wa maabara wa sampuli hizo unaendelea.

**ii. Mafunzo Ya Tathmini ya Maombi ya Majaribio Ya Chanjo**

Mafunzo ya namna ya kufanya tathmini (assessment) ya maombi ya majaribio ya chanjo *(vaccines clinical trials applications)* yalifanyika ambapo jumla ya washiriki 14 kutoka TMDA (4), Rwanda FDA (1), ZAHRI (2), ZFDA (3) na KCRI (4) walipatiwa mafunzo hayo.

**iii. Mafunzo ya Tathmini ya Maombi ya Majaribio ya Vifaa Tiba**

Mafunzo ya namna ya kufanya tathmini (assessment) ya maombi ya majaribio ya vifaa *(medical devices clinical investigation applications*) ambapo jumla ya washiriki 11 kutoka TMDA (2), Rwanda FDA (1), ZAHRI (2), ZFDA (5) na MUHAS (1).

**iv. Kikao cha Mwaka cha Wadau wa Mradi *(Annual Consortium Meeting)***

Kikao cha Mwaka cha Wadau wa Mradi *(Annual Consortium Meeting)* kilifanyika Zanzibar na kilihudhuriwa na washiriki 31 kutoka taasisi 8 kati ya 9 zinazoshiriki Mradi huu. Idadi ya washiriki kwa kila taasisi ni kama ifuatavyo; (ambao ni) ZFDA (11), TMDA (7), ZAHRI (5), KI (3), KCRI (2), NIMR (2), MUHAS (2) na Rwanda FDA (1). Taasisi ambayo haikushiriki ni University of St. Andrew, UK.

Maazimio ya kikao hicho yalijumuisha mambo yafuatayo ambayo tayari yameshatekelezwa;

- Kuhakikisha kwenye kila kazi ya Mradi, mhisani anatambuliwa (acknowledged).
- Taarifa za utekelezaji za nusu mwaka (Mid-Term Project report) iandaliwe kwa kujumuisha taarifa zote za fedha na kazi zote zilizofanyika tangu Mradi uanze;
- Kazi zote za Mradi zitekelezwe ndani ya muda uliopangwa.
- Wadau wote washirikishane kwenye utekelezaji wa kazi za Mradi;
- Sampuli zote zilizofanyiwa tathmini ya taarifa zake *(product information review)* ziwasilishwe maabara ya TMDA na kufanyiwa uchunguzi; Chuo cha MUHAS na Rwanda FDA kuhakikisha ***curriculum*** walizozianzisha zinapata ithibati. Curricular hizo ni za ***Bioethics course*** kwa Rwanda FDA na ***Training on in-vitro and medical devices Clinical Trial assessment*** na ***Training on rapid evaluation of vaccines trials; na***
- Kibali mahususi ***(Ethical clearance)*** cha Mradi kifuatiliwe na kuhakikisha upatikanaji wake.

Aidha Maazimio yote yametekelezwa na yanaendelea kuzingatiwa isipokuwa ***accreditation ya Bioethics course*** ambapo bado Rwanda FDA wanashughulikia.

**v. Kikao cha Kamati ya Uongozi *(Steering Committee)***

Kikao cha ***Steering Committee*** ya Mradi wa BREEDIME kilifanyika na kilihudhuriwa na taasisi zote 13 shiriki za Mradi ambazo ni TMDA (5), Karolinska Institute (3), Rwanda FDA (1) Muhimbili

University of Health and Allied Sciences (1), NIMR (1), Kilimanjaro Christian Research Institute (1) na Universtiy of St. Andrew, UK (1).

Katika Kikao hicho ilielezwa kuwa jumla ya kazi 20 (76.9%) kati ya 26 za Mradi huo zimetekelezwa. Kazi sita (6) zilizobakia zimeorodheshwa hapa chini na zitakamilishwa mwaka ujao wa fedha wa 2025/26.

- Tathmini Jumuishi ya Majaribio Dawa.
- Ithibati ya Kaguzi Jumuishi za Majaribio ya Dawa.
- Kuzijengea uwezo taasisi za Kiudhibiti za nchi shiriki wa Mradi na kushirikishana kwenye nyanja ya Sayansi.
- Tathmini na Ufuatiliaji wa Mradi.
- Kujenga ufahamu wa jamii juu ya uwepo wa Mradi.
- Utoaji wa taarifa kwa wadau wa Mradi.

Kikao hicho kiliazimia kuwa kazi zote zitekelezwe ndani ya muda uliopangwa na taasisi shiriki ziendelee kushirikiana.

### (d) Utekelezaji wa Mradi wa RER - CTO

Mamlaka tangu tarehe 1 Julai, 2024 imekuwa ikitekeleza Mradi wa miaka 3 unaoitwa ***""Reinforce the Ethical and Regulatory Ecosystem for the Transformation of Clinical Trials Oversight in Ethiopia, Tanzania and beyond" kwa ufupi*** "RER-CTO" wenye lengo la kuimarisha udhibiti Sera, Uwezo, Miundombinu na Ushirikiano katika Udhibiti wa majaribio ya dawa, chanjo na vifaa tiba.

Mradi huo unatekelezwa kwa kushirikiana na taasisi zingine 7 ambazo ni; *University of Oslo (UiO), Norway, Armauer Hansen Research Institute (AHRI), Ethiopia; Ethiopian Food and Drugs Authority (EFDA), Ethiopia; Karolinska Institute (KI), Sweden; Ministry of Education (MoE), Ethiopia; National Institute for Medical Research (NIMR), Tanzania.*

Aidha katika Mradi huo Mamlaka ilipewa jukumu la kusimamia kuanzishwa kwa mfumo wa kielektoriniki kwa EFDA na AHRI na uboreshaji wa Mifumo ya kielektroniki kwa TMDA na NIMR inayotumika kudhibiti majaribio ya dawa, chanjo na vifaa tiba na maadili wakati wa tafiti. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Juni, 2025 Mamlaka imetekeleza kazi **2** za Mradi huo;

i. Kutengeneza vitendea kazi (Tools) kwa ajili ya kufanya tathmini za mahitaji ya kutengeneza na kuboresha mifumo ya kielektroniki (digitalization need assessment tool) katika taasisi za EFDA, AHRI, TMDA na NIMR,

ii. Kutengeneza mahitaji ya watumiaji (user requirement specification) kwa ajili ya kuanzisha na kuboresha mifumo ya kielektroniki (digitalization need assessment tool) katika taasisi za EFDA, AHRI, TMDA na NIMR,

iii. Kupitia na kufanya maboresho ya Miongozo ya Udhibiti wa Majaribio ya Dawa, Chanjo na Vifaa Tiba ambapo jumla ya Miongozo mitatu (3) ilifanyiwa maboresho kwa kuzingatia mapungufu ambayo yamekuwa yakionekana katika vipindi tofauti tofauti vya utekelezaji wa miongozo hiyo pamoja na matokeo ya dodoso lililotolewa kwa Watumiaji wa Miongozo hiyo. Miongozo iliyofanyiwa maboresho ni:-

- Mwongozo wa Maombi ya Kuendesha Majaribio ya Dawa wa mwaka 2022;
- Mwongozo wa Uwekaji Dhamana na Ulipaji wa Fidia kwa Washiriki wa Majaribio, wa mwaka 2010; na
- Mwongozo wa Ukaguzi wa Majaribio ya Dawa wa mwaka 2020.

## (e) Utekelezaji wa Mradi wa Grand Challenge

Kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2024 TMDA ilianza kutekeleza Mradi wa *Grand Challenge* chini ya ufadhili wa *Bill and Melinda Gates Foundation*. Mradi huu wa miaka miwili (2) unaotarajiwa kuisha 30 Septemba, 2026 unashirikisha nchi 3 ambazo ni Tanzania, Rwanda na Ethiopia unalenga pamoja na kazi nyingine za kiudhibiti kuimarisha mifumo ya kielektroniki ya udhibiti wa majaribio ya dawa na chanjo baina ya nchi hizo.

Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Juni, 2025 Mamlaka ilitekeleza kazi moja ya Mradi huo ambayo ni kuandaa mahitaji ya kimfumo ili kuboresha moduli ya udhibiti wa majaribio ya Dawa katika mfumo wa Taasisi wa RIMS pamoja na kuainisha viashiria nane (8) vya msingi (*Key performance Indicators*) vya utendaji kazi ambavyo vitaweza kutolewa taarifa moja kwa moja kupitia mfumo. Aidha mahitaji ya watumiaji (user specification requirements – URS) yaliainishwa.



# 2.0 KUHAKIKISHA USALAMA, UBORA NA UFANISI WA VIFAA TIBA NA VITENDANISHI

Mamlaka imepewa jukumu la udhibiti wa vifaa tiba na vitendanishi kwa ajili ya kuhakikisha bidhaa hizo ni bora, salama na zenye ufanisi ili kulinda afya ya jamii kwa kuzuia athari ambazo zinaweza kujitokeza kutokana na matumizi yake.

Katika kutekeleza jukumu hilo, Mamlaka kupitia Kurugenzi ya Vifaa tiba na Vitendanishi imeendelea kufanya usajili, ukaguzi na kutoa leseni kwa viwanda vya ndani na maeneo ya biashara ya bidhaa hizo.

Vilevile, Mamlaka imeendelea kufuatilia madhara yatokanayo na matumizi ya vifaa tiba na vitendanishi pamoja na kufuatilia ubora na usalama wa bidhaa hizo katika soko. Kazi zilizotekelezwa ni kama zilivyoainishwa katika dondoo **2.1.1-2.2.3** hapa chini:

## 2.1.1 Usajili wa Vifaa Tiba na Vitendanishi

Jumla ya maombi 439 ya vifaa tiba (mapya 325 na huisha 114) yalipokelewa sawa na 121% ya lengo la maombi 362. Vilevile, maombi 51 ya mabadiliko yalipokelewa sawa na 165% ya lengo la maombi 31 kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na.24** na **23B**

Aidha, jumla ya maombi 262 ya vitendanishi (mapya 179 na huisha 83) yalipokelewa sawa na 218% ya lengo la maombi 120. Vilevile, maombi 25 ya mabadiliko yalipokelewa sawa na 156% ya lengo la maombi 16 kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na.24** na **23B.**

**Jedwali Na. 23A: Idadi ya Maombi ya Usajili wa Bidhaa za Vifaa Tiba na Vitendanishi Yaliyopokelewa Ukilinganisha na Maoteo kwa Mwaka 2024/25**

| Na | Bidhaa | Lengo | Pokelewa | % |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Vifaa Tiba | 362 | 454 | 121 |
| 2. | Vitendanishi | 120 | 272 | 218 |
| **Jumla Kuu** | | **482** | **726** | **145** |

**Jedwali Na. 23B: Idadi ya Maombi ya Usajili wa Bidhaa za Vifaa Tiba na Vitendanishi (Mabadiliko) Yaliyopokelewa Ukilinganisha na Maoteo kwa Mwaka 2024/25**

| Na | Bidhaa | Lengo | Pokelewa | % |
|---|---|---|---|---|
| | Vifaa Tiba | 31 | 51 | 165 |
| | Vitendanishi | 16 | 25 | 156 |
| **Jumla Kuu** | | **47** | **76** | **162** |

Kuvuka kwa lengo kwa upande wa maombi ya usajili wa Vifaa Tiba na Vitendanishi kumechangiwa na ongezeko la uelewa kwa wafanyabiashara juu ya umuhimu wa kufuata taratibu za usajili wa vifaa tiba.

Pamoja na kupokea maombi mapya ya usajili, kuhuisha na mabadiliko, Mamlaka pia ilipokea majibu ya hoja 726 (454 ya vifaa tiba, 272 vitendanishi) kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali** Na.**25**

Vilevile, kulikuwa na salio la maombi 14 ya vifaa tiba (mapya 4 na hoja 10) na maombi 8 ya vitendanishi (mapya 5 na hoja 3) kutoka mwaka uliopita 2023/2024, hivyo kufanya jumla ya maombi yote yaliyokuwepo kuwa 1426 ambapo jumla ya maombi 1403 sawa na 98% ya maombi yote yaliyokuwepo yalifanyiwa tathmini.

Mchanganuo wa matokeo ya tathmini kwa aina mbalimbali za maombi ya usajili wa vifaa tiba na vitendanishi ni kama yalivyoainishwa katika dondoo **2.1.2 -2.1.7**

## 2.1.2 Tathmini na Usajili wa Vifaa Tiba

Katika kipindi cha mwaka 2024/2025 jumla ya maombi 439 (mapya 325 na huisha 114) yalipokelewa. Aidha, kulikuwa na maombi mapya manne (4) yaliyobaki hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2024 na hivyo kufanya jumla ya maombi yote kuwa 443 (mapya 329 na huisha 114).

Kati ya maombi mapya 325 yaliyopokelewa, maombi 74 (23%) yalikuwa ya daraja A, maombi 113 (35%) ya daraja B, maombi 106 (33%) ya daraja C na maombi 31 (9%) ya daraja D. Kati ya maombi hayo yaliyopokelewa ombi moja (1) lilikuwa ni la kifaa tiba cha ndani ya nchi aina ya BP CPAP *Machine*.

Idadi hii ni ongezeko la maombi 53 (19%) ukilinganisha na maombi 272 yaliyopokelewa kufikia tarehe 30 Juni 2024 kwa mwaka 2023/24. Kati ya maombi hayo yaliyopokelewa katika mwaka 2023/24 maombi ya ndani ya nchi yalikuwa manne (4) ambapo daraja A ombi moja (1), daraja B maombi mawili (2) na daraja C ombi moja (1). Aidha, ongezeko la maombi ya usajili wa vifaa tiba katika kipindi hiki limechangiwa na ongezeko la uelewa kwa wafanyabiashara juu ya umuhimu wa kufuata taratibu za usajili wa vifaa tiba.

Katika kipindi hiki maombi mengi yaliyopokelewa ni ya vifaa tiba vya daraja B na daraja C ambapo vifaa tiba vya Daraja B vilivyopokelewa kwa wingi katika kipindi hiki ni *surgical gloves, autodisable syringes, infusion set, ultrasound system* na *iv cannula*. Kwa upande wa vifaa tiba daraja C vilivyopokelewa na kusajiliwa zaidi ni *non absorbable sutures, male condoms, diagnostic x-rays* na *hemodialysis system.*

Maombi ya daraja C yameongezeka kwa 41% ukilinganisha na mwaka 2023/24 hii ni kwa sababu ya mapinduzi makubwa katika uboreshaji wa huduma za afya na kuanzishwa kwa huduma za upasuaji katika vituo vya afya, ujenzi wa majengo ya dharura, kuanzishwa kwa huduma za kuchuja damu kwa wagonjwa wa magonjwa sugu ya figo katika hospitali za rufaa za mikoa, usimikaji wa mitambo ya radiologia na ukuaji wa teknologia. Ulinganifu wa maombi yaliyopokelewa kwa madaraja umeainishwa kwenye **Mchoro Na. 1**

**Mchoro Na. 1: Ulinganifu wa Madaraja ya Vifaa Tiba Vilivyopokelewa**




Jumla ya maombi 432 sawa na 97.5% ya maombi yaliyokuwepo yalifanyiwa tathmini, kati ya hayo maombi 255 (59%) (mapya 187 na kuhuisha 68) yaliidhinishwa, na maombi 180 (41.6%) (mapya 131 na huisha 49) yalikuwa na hoja na maombi mapya 11 yamebaki hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2025. Maombi yaliyobaki yatafanyiwa tathmini kwa kipindi kinachofuata na hapakuwa na ombi lolote la usajili wa vifaa tiba lililokataliwa kama ilivyooneshwa katika mchoro Na.1.

Aidha, kuna ongezeko la maombi yaliyofanyiwa tathmini na kuidhinishwa ukilinganisha na kipindi cha 2023/24, ambapo maombi 236 yalifanyiwa tathmini na maombi 166 yaliidhinishwa. Ulinganifu umeoneshwa kwenye mchoro Na.2. Ongezeko la maombi yaliyofanyiwa tathmini na yaliyoidhinishwa yanaonesha ongezeko la ufanisi katika utendaji kazi ambao pia umechangiwa na ongezeko la watumishi wapya walioajiriwa na kufanyiwa mafunzo.

**Mchoro Na. 2: Ulinganifu wa Madaraja ya Vifaa Tiba Vilivyofanyiwa Tathmini**



## 2.1.3 Tathmini na Usajili wa Vitendanishi

Katika kipindi cha mwaka 2024/2025 jumla ya maombi 262 (mapya 179 na huisha 83) yalipokelewa. Aidha, kulikuwa na maombi mapya matano (5) yaliyobaki hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2024 na hivyo, kufanya maombi yote kuwa 267 (mapya 184 na huisha 83).Ulinganifu wa maombi yaliyopokelewa kwa madaraja:

**Daraja A:** Maombi yaliongezeka kwa 292% kutoka 12 (2023/24) hadi 47 (2024/25)

**Daraja B:** Maombi yaliongezeka kwa 56% kutoka maombi 36 (2023/24) hadi 56 (2024/25).

**Daraja C:** Maombi pia yameongezeka kwa 153% kutoka 19 (2023/24) hadi 48(2024/25).

**Daraja D:** Maombi yaliongezeka kwa 18% kutoka maombi 22 (2023/24) hadi 26 (2024/25).

**Mchoro Na. 3 : Ulinganifu wa Madaraja ya Vitendanishi Vilivyopokelewa**




Jumla ya maombi 249 sawa na 93% ya maombi yote yaliyokuwepo yalifanyiwa tathmini. Kati ya hayo maombi 143 sawa na 57% yaliidhinishwa. Maombi 101 (mapya 71 na huisha 30) yalikuwa na hoja na maombi mapya 18 yamebaki hadi kufikia tarehe 30 Juni 2025. Maombi yaliyobaki yatafanyiwa tathmini kwa kipindi kinachofuata na hapakuwa na ombi lolote la usajili wa vitendanishi lililokataliwa kama ilivyooneshwa katika **jedwali Na. 24.**

## 2.1.4 Tathmini na Usajili wa Maombi Mengine ya Vifaa Tiba

Jumla ya maombi 531 (mabadiliko 51, matangazo 26 na majibu ya hoja 454) yanayohusu usajili wa vifaa tiba yalipokelewa na kulikuwa na maombi 10 ya majibu ya hoja yaliyobaki hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2024 na hivyo kufanya jumla ya maombi yote kuwa 541 (matangazo 26, mabadiliko 51 na majibu ya hoja 464). Jumla ya maombi 497 (mabadiliko 51, matangazo 26 na majibu ya hoja 420) sawa na 92% yalifanyiwa tathmini ambapo maombi 50 (mabadiliko 33 na matangazo 17) yaliidhinishwa na maombi 28 (mabadiliko 17 na matangazo 9) yalikuwa na hoja na maombi 44 ya majibu ya hoja yamebaki hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2025 kama ilivyoonyeshwa katika **Jedwali Na. 25**

### 2.1.5 Tathmini na Usajili wa Maombi Mengine ya Vitendanishi

Jumla ya maombi 299 (matangazo 2, mabadiliko 25 na majibu ya hoja 272) yanayohusu usajili wa vitendanishi yalipokelewa. Aidha, kulikuwa na maombi matatu (3) ya majibu ya hoja yaliyobaki hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2024 na hivyo kufanya jumla ya maombi yote kuwa 307 (matangazo 2, mabadiliko 25 na majibu ya hoja 280).

Jumla ya maombi 297(matangazo 2, mabadiliko 25 na majibu ya hoja 280) sawa na 97% yalifanyiwa tathmini ambapo maombi 15 (matangazo 1 na mabadiliko 14) yaliidhinishwa na maombi 122 (matangazo 1, mabadiliko 11 na majibu ya hoja 110) yalikuwa na hoja ambapo maombi 10 ya majibu ya hoja yamebaki hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2025 kama ilivyoonyeshwa katika **Jedwali Na.25.**

### 2.1.6 Tathmini ya Maombi ya Utambuzi wa Vifaa Tiba na Vitendanishi

Jumla ya maombi 1,200 ya utambuzi (vifaa tiba 1,000 na vitendanishi 200) yalipangwa kupokelewa na kufanyiwa tathmini katika kipindi cha mwaka 2024/2025. Jumla ya Maombi 1477 (vifaa tiba 1323 na vitendanishi 154) ya utambuzi wa vifaa tiba na vitendanishi yalipokelewa na kulikuwa na maombi manne (4) ya vifaa tiba yaliyobaki hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2024 na kufanya jumla ya maombi ya utambuzi kwa mwaka kuwa 1439 (vifaa tiba 1339 na vitendanishi 154).

Jumla ya maombi 1475 (vifaa tiba 1325 na vitendanishi 148) yalifanyiwa tathmini ambapo maombi 1280 (vifaa tiba 1191 na vitendanishi 89) yaliidhinishwa, na maombi 191 (vifaa tiba 132 na vitendanishi 59) yalikuwa na hoja na maombi 20 (vifaa tiba 14 na vitendanishi 6) yamebaki, mchanganuo ni kama ilivyoonyeshwa katika **Jedwali Na. 26.**

Ulinganifu wa maombi ya utambuzi wa vifaa tiba unaonyesha ongezeko la maombi 540 (69%) kwa mwaka wa fedha 2024/25, kutoka maombi 783 hadi 1323. Maombi ya utambuzi wa vitendanishi yameongezeka kwa 190% kutoka 53 hadi 154 kwa mwaka 2024/25.

Ongezeko hili linaashiria kuongezeka kwa uingizaji wa vifaa tiba na vitendanishi vyenye uhatarishi mdogo, hasa kutokana na matumizi yake ya mara moja (single use). Vifaa vilivyowasilishwa kwa maombi mengi ni pamoja na *baby diapers* na *sanitary pads* na kwa upande wa vitendanishi ni *reagents* na *culture media*.

Vifaa tiba vilivyotengenezwa ndani ya nchi na kuombewa utambuzi kwa wingi ni pamoja na: *Delivery kits, Sanitary pads,* Vitanda vya hospitali (hospital beds), Magogo ya kubebea wagonjwa (hospital stretchers), *Baby diapers* na viti vya kuchangia damu (blood donation chairs).

Jedwali Na. 24:Mchanganuo wa Tathmini na Usajili wa Maombi ya Bidhaa

| Na | Aina ya bidhaa | Maelezo | Baki ya Juni 30, 2024 | Pokelewa | Jumla | Tathminiwa | Idhinishwa | Kataliwa | Hoja | Baki |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Vifaa tiba | Mapya | 4 | 325 | **329** | 318 | 187 | 0 | 131 | 11 |
| | | Huisha | 0 | 114 | **114** | 114 | 68 | 0 | 49 | 0 |
| | | **Jumla ndogo** | **4** | **439** | **443** | **432** | **255** | **0** | **180** | **11** |
| 2. | Vitendanishi | Mapya | 5 | 179 | **184** | 166 | 90 | 0 | 76 | 18 |
| | | Huisha | 0 | 83 | **83** | 83 | 53 | 0 | 30 | 0 |
| | | **Jumla ndogo** | **5** | **262** | **267** | **249** | **143** | **0** | **106** | **18** |
| **Jumla Kuu** | | | **9** | **701** | **710** | **681** | **398** | **0** | **286** | **29** |

Jedwali Na. 25: Mchanganuo wa Maombi Mengine Yanayohusu Usajili wa Bidhaa

| Na | Aina ya bidhaa | Maelezo | Baki ya Juni 30, 2024 | Pokelewa | Jumla | Tathminiwa | Idhinishwa | Kataliwa | Hoja | Baki |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Vifaa tiba | Matangazo | 0 | 26 | **26** | 26 | 17 | 0 | 9 | 0 |
| | | Mabadiliko | 0 | 51 | **51** | 51 | 33 | 0 | 19 | 0 |
| | | Majibu ya Hoja | 10 | 454 | **464** | 420 | 0 | 0 | 230 | 44 |
| | | **Jumla ndogo** | **10** | **531** | **541** | **497** | **50** | **0** | **258** | **44** |
| 2. | Vitendanishi | Matangazo | 0 | 2 | **2** | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 |
| | | Mabadiliko | 0 | 25 | **25** | 25 | 14 | 0 | 11 | 0 |
| | | Majibu ya Hoja | 3 | 272 | **280** | 270 | 0 | 0 | 110 | 10 |
| | | **Jumla ndogo** | **3** | **299** | **307** | **297** | **15** | **0** | **122** | **10** |
| **Jumla Kuu** | | | **13** | **830** | **848** | **794** | **65** | **0** | **380** | **54** |

Jedwali Na. 26: Mchanganuo wa Maombi ya Utambuzi wa Vifaa Tiba na Vitendanishi

| Na | Aina ya bidhaa | Maelezo | Baki ya Juni 30, 2024 | Pokelewa | Jumla | Tathminiwa | Idhinishwa | Kataliwa | Hoja | Baki |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Vifaa tiba | Mapya | 4 | 1323 | 1339 | 1325 | 1191 | 0 | 132 | 14 |
| 2. | Vitendanishi | Mapya | 0 | 154 | 154 | 148 | 89 | 0 | 59 | 6 |
| **Jumla Kuu** | | | **4** | **1477** | **1493** | **1473** | **1280** | **0** | **191** | **20** |

## 2.1.7 Usajili wa Maeneo na Utoaji wa Vibali vya Biashara ya Vifaa Tiba na Vitendanishi

Mfumo wa usajili wa maeneo ya biashara za bidhaa za vifaa tiba na vitendanishi husaidia kuhakikisha kuwa maeneo husika yanakidhi vigezo ili kutoathiri usalama, ubora na ufanisi wa bidhaa tajwa. **Jedwali Na. 27** linaonesha mchanganuo wa usajili wa maeneo ya biashara ya vifaa tiba.

**Jedwali Na. 27: Maombi ya Usajili wa Maeneo na Utoaji wa Vibali vya Biashara ya Vifaa Tiba na Vitendanishi**

| Aina ya jengo | | | Baki 2023/2024 | Yaliyopokelewa | | Jumla | Yaliyotathminiwa | Yaliyosajiliwa | Vibali vilivyotolewa | Kataliwa/Hoja | % yaliyokidhi vigezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mapya | Huisha | | | | | | |
| Vifaa tiba | Viwanda vya ndani | Vikubwa | 0 | 1 | 3 | 4 | 4 | 4 | 4 | 0 | 100.0 |
| | | Kati | 0 | 8 | 18 | 26 | 26 | 21 | 21 | 5 | 80.8 |
| | | Vidogo | 0 | 6 | 8 | 14 | 14 | 11 | 11 | 3 | 78.6 |
| | **Jumla ndogo** | | **0** | **15** | **29** | **44** | **44** | **36** | **36** | **8** | **81.8** |
| Vifaa tiba na vitendanishi | Maduka ya Jumla | | 0 | 164 | 344 | 508 | 508 | 490 | 490 | 18 | 96.5 |
| | Maduka ya rejereja | | 0 | 31 | 44 | 75 | 74 | 65 | 65 | 10 | 87.8 |
| | Magari ya kubebea vifaa tiba | | 0 | 2 | 0 | 2 | 2 | 2 | 2 | 0 | 100.0 |
| | **Jumla ndogo** | | **0** | **197** | **388** | **585** | **584** | **557** | **557** | **28** | **95.3** |
| Gesi tiba | Viwanda | | 0 | 1 | 1 | 2 | 2 | 1 | 1 | 1 | 50.0 |
| | Hospitali | | 0 | 0 | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 0 | 100.0 |
| | Wauzaji wa jumla | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| | **Jumla ndogo** | | **0** | **1** | **2** | **3** | **3** | **2** | **2** | **1** | **66.7** |
| **JUMLA KUU** | **Jumla Kuu** | | **0** | **213** | **419** | **632** | **631** | **595** | **595** | **37** | **94.3** |

Kwa mujibu wa **Jedwali Na. 27:** Mamlaka ilipokea jumla ya maombi yote 632 ya usajili wa maeneo ya biashara ya vifaa tiba na vitendanishi. Maombi 631 yalifanyiwa kazi ambapo maeneo 595 (94%) yalikidhi vigezo na kusajiliwa. Maeneo yaliyofanyiwa tathmini ni pungufu ya maeneo 30 (4.5%) ikilinganishwa na maeneo 661 yaliyotathminiwa mwaka uliopita. Vilevile, maeneo yaliyokidhi vigezo ni ongezeko la maeneo 6 ikilinganishwa na maeneo 589 yaliyokidhi vigezo katika kipindi kama hiki mwaka uliopita.

## 2.1.8 Ukaguzi wa Viwanda na Maeneo ya Biashara za Vifaa Tiba, Vitendanishi na Gesi Tiba

Viwanda na maeneo ya biashara za vifaa tiba, vitendanishi na gesi tiba hukaguliwa wakati wowote ili kuhakiki ubora wa majengo, mifumo ya utengenezaji na mazingira ya uzalishaji, usambazaji, uhifadhi na uuzaji ili kudhibiti ubora na usalama wa bidhaa hizi.

Mamlaka hukagua viwanda na maeneo yote yanayojihusisha na uendeshaji wa biashara ya bidhaa husika ikiwa ni pamoja na magari ya kubeba bidhaa hizi. Mchanganuo wa ukaguzi wa viwanda na maeneo ya biashara za vifaa tiba, vitendanishi na gesi tiba umeainishwa katika dondoo **2.1.8 - 2.2.10**

## 2.1.9 Ukaguzi wa Viwanda vya Kati, Vidogo na Meneo ya Biashara

Ukaguzi wa viwanda vya kati, vidogo na maeneo ya biashara za vifaa tiba na vitendanishi umeainishwa katika **Jedwali Na. 28** hapa chini.

**Jedwali Na. 28: Ukaguzi wa Viwanda vya Ndani na Maeneo ya Biashara za VifaaTiba**

| Aina ya Biashara | | | Yaliyopangwa Kukaguliwa | Yaliyokaguliwa | | Yaliyokidhi Vigezo | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Idadi | % | Yaliyosajiliwa | Yasiyosajiliwa | Jumla | % |
| Vifaa tiba na Vitendanishi | Viwanda vya ndani | Kati | 2 | 3 | 150 | 3 | 0 | **3** | **100** |
| | | Vidogo | 46 | 46 | 100 | 46 | 0 | **46** | **100** |
| | Maduka ya Jumla | | 338 | 308 | 91 | 295 | 7 | **302** | **98** |
| | Maduka ya reja reja | | 47 | 85 | 180 | 85 | 0 | **85** | **100** |
| | Maghala | | 4 | 8 | 200 | 6 | 0 | **6** | **75** |
| | Maabara | | 1028 | 1014 | 98 | 877 | 6 | **883** | **87** |
| | Magari ya kubebea Vifaa tiba | | 2 | 19 | 950 | 19 | 0 | **19** | **100** |
| Gesi Tiba | Wauzaji wa Rejareja | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** | **0** |
| | Wauzaji wa jumla | | 12 | 21 | 175 | 19 | 0 | **19** | **90** |
| **JUMLA KUU** | | | **1479** | **1504** | **102** | **1350** | **13** | **1363** | **91** |

Kwa mujibu wa **Jedwali Na.28** kati ya maeneo 1,504 yaliyokaguliwa, maeneo 1,363 (91%) yalikidhi vigezo. Maelekezo ya kuboresha maeneo yasiyokidhi vigezo yalitolewa kwa wamiliki na wasimamizi wa maeneo tajwa kwa ajili ya ufuatiliaji. Maeneo yaliyokaguliwa ni pungufu ya maeneo 831 ikilinganishwa na maeneo 2,335 yaliyokaguliwa katika mwaka uliopita. Vilevile, maeneo yaliyokidhi vigezo ni pungufu ya maeneo 752 ikilinganishwa na maeneo 2,115 yaliyokidhi vigezo mwaka uliopita.

## 2.2.0 Ukaguzi wa Viwanda Vikubwa vya Ndani

Jumla ya viwanda vya ndani 19 vilivyopo nchini vinavyojihusisha na utengenezaji wa vifaa tiba na vitendanishi vilipangwa kukaguliwa ambapo 16 ni vya vifaa tiba na 3 vitendanishi. Katika kipindi cha Julai 2024 – Juni, 2025 viwanda vyote 19 vimekaguliwa na vilikidhi viwango vya ubora. Ukaguzi huo ulikuwa ni wa ufuatiliaji (follow-up inspection). Hakukuwa na maombi mapya ya viwanda vya ndani yaliyopokelewa, kama inavyoonyeshwa kwenye **Jedwali Na. 29**

**Jedwali Na. 29.Ukaguzi wa Viwanda vya Ndani na Maeneo ya Biashara za Vifaa Tiba na Vitendanishi**

| Aina ya kiwanda | Yaliyopokelewa | Yaliyokaguliwa | Yenye hoja | Yaliyokidhi matakwa | Yaliyosajiliwa | Ambavyo havijaanza uzalishaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Vifaa Tiba | 0 | 16 | 0 | 16 | 16 | 0 |
| Vitendanishi | 0 | 3 | 0 | 3 | 3 | 0 |
| Jumla | 0 | 19 | 0 | 19 | 19 | 0 |

### 2.2.1 Ukaguzi wa Viwanda vya Kutengeneza Gesi Tiba

Ukaguzi wa mitambo ya kuzalisha gesi ulifanyika katika viwanda 22. Kati ya hivyo, viwanda vitano (5) vilibainika kuwa na hoja zinazohitaji kufanyiwa kazi, huku viwanda kumi na saba (17) vikikidhi viwango vya ubora. Ombi moja (1) pekee ndilo lilikuwa jipya, na linatoka katika Kanda ya Kaskazini, kama inavyoonyeshwa kwenye **Jedwali Na. 30** hapa chini;

**Jedwali Na. 30: Ukaguzi wa Viwanda vya Kutengeneza Gesi Tiba**

| Kanda | Yaliyopokelewa | Yaliyokaguliwa | Yenye hoja | Yaliyokidhi |
|---|---|---|---|---|
| Mashariki | 0 | 5 | 1 | 4 |
| Nyanda za Juu Kusini | 0 | 4 | 1 | 3 |
| Kaskazini | 1 | 4 | 1 | 3 |
| Ziwa Mashariki | 0 | 5 | 1 | 4 |
| Kati | 0 | 4 | 1 | 3 |
| **Jumla** | **1** | **22** | **5** | **17** |

### 2.2.2 Ukaguzi wa Viwanda vya Vifaa Tiba na Vitendanishi Nje ya Nchi

Jumla ya maombi 47 ya ukaguzi wa viwanda yalipangwa kupokelewa, ikiwa maombi 35 kutoka Asia, 5 Ulaya, 3 America, 2 Afrika Mashariki na 2 Afrika nje ya Afrika Mashariki. Jumla ya maombi ya ukaguzi wa viwanda 59 (125%) yalipokelewa ambapo 52 vifaa tiba na 07 vitendanishi. Vilevile kulikuwa na maombi ya ukaguzi wa viwanda 41 (24 vifaa tiba na 17 vitendanishi) yaliyobaki kufikia tarehe 30 Juni, 2024, hivyo kufanya jumla ya maombi yote kuwa 100 (76 vifaa tiba na 24 vitendanishi). Jumla ya viwanda 32 vilipangwa kukaguliwa ana kwa ana, na viwanda 15 vilipangwa kukaguliwa kwa njia ya dawati. Viwanda 42 vilikaguliwa ambapo viwanda 29 vilifanyiwa ukaguzi wa ana kwa ana na 13 kwa njia ya dawati sawa na 89% ya viwanda vilivyopangwa kukaguliwa.

Mchanganuo wa viwanda hivyo unaonekana kwenye **jedwali Na. 31** hapa chini.

**Jedwali Na. 31: Ukaguzi wa Viwanda vya Vifaa Tiba na Vitendanishi Nje ya Nchi Mwaka 2024-2025**

| Aina ya Viwanda | Baki kutoka 2023-2024 | Maombi yaliyopokelewa | Jumla | Ukaguzi wa ana kwa ana | Kwa njia ya dawati | jumla ya baki |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Vifaa Tiba | 24 | 52 | **76** | 24 | 11 | **41** |
| Vitendanishi | 17 | 07 | **24** | 05 | 02 | **17** |
| **Jumla** | **41** | **59** | **100** | **29** | **13** | **58** |

### 2.2.3 Udhibiti wa Uingizaji Nchini na Usafirishaji Nje ya Nchi wa Vifaa Tiba na Vitendanishi

Mamlaka ilipanga kupokea jumla ya maombi 10,960 (10,000 kuingiza, 800 kutoa na 160 malighafi). Katika kipindi hiki, maombi 10,416(87%) (9056 kuingiza, 1066 kutoa, 294 malighafi) ya kuingiza na kutoa nje ya nchi vifaa tiba na vitendanishi yalipokelewa. Kati ya maombi yaliyopokelewa 9,306 (8014 kuingiza, 1011 kutoa, 281 malighafi) yaliidhinishwa na ambayo hayakuidhinishwa yalikuwa na hoja.

Aidha, katika vibali 9350 vya kuingiza bidhaa nchini, 1989 vilikuwa vibali vya kawaida, 7067 (76%) vibali maalum na 294 vibali vya kuingiza malighafi. katika kipindi hiki vibali maalum vimeendelea kutolewa kwa wingi kutokana na kuwa na kiasi kikubwa cha vifaa vya msaada (donation), vituo vya kutolea huduma kuruhusiwa kuingiza bidhaa moja kwa moja bila kusajili na *accessories* na *reagents* zilizosajiliwa pamoja na vifaa hazipatikani kwenye *portal* ya mteja hivyo kulazimika kuomba vibali maalumu.

Tathmini ya maombi ya vibali vya kuingiza vifaa tiba na vitendanishi nchini kwa mwaka huu 2024/25 inaonyesha kuwa idadi ya maombi ya vibali yaliyopokelewa yameongezeka kwa maombi 603 (7%) ikilinganishwa na kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024, ambapo maombi yaliyoidhinishwa ni 7696(91%) ya yale yaliyopokelewa 8453.

Hata hivyo idadi ya vibali vilivyokaguliwa kwenye vituo vya forodha ilikuwa 6834 (73%) sawa na upungufu wa 27% kutoka kwenye idadi ya vibali vilivyoidhinishwa hii ni kutokana na kuwa siyo kila kibali kinakaguliwa katika kipindi kile kile kilicho tolewa bali hutegemea muda wa kufika nchini kwa shehena. Mchanganuo wa maombi hayo ni kama ulivyoainishwa kwenye **Jedwali Na.32**.

**Jedwali Na. 32: Maombi ya Vibali vya Kuingiza Nchini na Kusafirisha Bidhaa Nje ya Nchi**

| Na | Aina ya bidhaa | Yaliyopokelewa | | Vibali vilivyoidhinishwa | | Vibali vilivyokaguliwa katika vituo vya forodha | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kuingia | Kutoka | Kuingia | Kutoka | Kuingia | Kutoka |
| 1. | Vifaa Tiba na Vitendanishi (Kawaida) | 1989 | 476 | 1902 | 474 | 6150 | 441 |
| 2. | VifaaTiba na Vitendanishi (Maalum) | 7067 | 590 | 6112 | 537 | | |
| 3. | Malighafi za Vifaa Tiba | 294 | 0 | 281 | 0 | 243 | 0 |
| **Jumla** | | **9350** | **1066** | **8295** | **1011** | **6393** | **441** |

# 2.2.4. Ufuatiliaji wa Usalama wa Vifaa Tiba na Vitendanishi

## 2.2.4.1 Ufuatiliaji Ubora na Ufanisi wa Vifaa Tiba wa Vitendanishi Kupitia Upimaji wa Toleo kwa Toleo Kabla ya Kusambazwa

Utaratibu wa upimaji toleo kwa toleo kwa baadhi ya vifaa tiba na vitendanishi ulianzishwa kwa lengo la kuhakikisha kuwa bidhaa zilizoainishwa na zinazoweza kuleta athari kubwa kwa afya ya Umma zina ubora unaokubalika na kufanya kazi kama ilivyokusudiwa na watengenezaji kwa kufanya uchunguzi wa maabara kabla ya kusambazwa kwa matumizi.

Katika kipindi hiki, jumla ya matoleo 255 ambapo 178 ni vifaa tiba na 77 ni vitendanishi yalichunguzwa katika uchunguzi wa toleo kwa toleo, ukilinganisha na kipindi cha mwaka 2023/2024 ambapo jumla ya matoleo 595 (477 ni vifaa tiba na 118 ni vitendanishi) yalichunguzwa.

Hali hii inaonesha kuwa mwaka 2024/2025 Mamlaka ilichunguza matoleo machache kuliko mwaka 2023/2024, hii imesababishwa kwa kiasi kikubwa na kupungua kwa uingizwaji wa mipira ya kiume aina ya Zana Male *Condoms* ambayo huingizwa na MSD.

Mchanganuo wa **mchoro Na. 4** unaonesha Mlinganyo wa matoleo ya vifaa tiba na vitendanishi yaliyofanyiwa uchunguzi kwa mwaka 2023/2024 na mwaka 2024/*2025* na idadi ya matoleo yaliyopokelewa, yaliyofanyiwa uchunguzi na matokeo ya uchunguzi yameoneshwa kwenye **Jedwali Na. 33A** na **Na. 33B**.

**Mchoro Na. 4: Mlinganyo wa Matoleo ya Vifaa Tiba na Vitendanishi Yaliyofanyiwa Uchunguzi kwa Mwaka 2023/2024 na Mwaka 2024/2025**




**Jedwali Na. 33A: Idadi ya Matoleo ya Vifaa Tiba Yaliyofanyiwa Uchunguzi**

| Na | Jina la kifaa tiba | Yaliyopokelewa | Yaliyofanyiwa uchunguzi | Yaliyofaulu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Zana male Condoms | 86 | 86 | 86 - yamefaulu |
| 2. | Contempo Condoms | 20 | 20 | 20 - yamefaulu |
| 3. | Skyn Male Condoms | 4 | 4 | 4 - yamefaulu |
| 4. | Bull Male Condoms | 10 | 10 | 10 - yamefaulu |
| 5. | Kiss Male Condoms | 24 | 24 | 24 - yamefaulu |
| 6. | Dume Male Condoms | 20 | 20 | 20 - yamefaulu |
| 7. | Fiesta Male Condoms | 3 | 3 | 3 - yamefaulu |
| 8. | Lifeguard Male Condoms | 5 | 5 | 5 - yamefaulu |
| 9. | Mood Male Condoms | 1 | 1 | 1 - limefaulu |
| 10. | Durex Male Condoms | 4 | 4 | 4 - yamefaulu |
| 11. | Female Condom | 1 | 1 | 1 - limefaulu |
| **Jumla** | | **178** | **178** | **178** |

**Jedwali Na.33B: Idadi ya Matoleo ya Vitendanishi Yaliyofanyiwa Uchunguzi**

| Na | Jina la kifaa tiba | Yaliyopokelewa | Yaliyofanyiwa uchunguzi | Yaliyofaulu |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Bioline HIV RDT | 33 | 33 | 33 - yamefaulu |
| 2 | Bioline HIV/Syphilis Duo RDT | 19 | 19 | 19 - yamefaulu |
| 3 | Oraquick HIV Self Test | 3 | 3 | 3 - yamefaulu |
| 4 | CheckNow HIV Self Test | 8 | 8 | 8 - yamefaulu |
| 5 | Meriscreen mRDT | 6 | 6 | 6 - yamefaulu |
| 6 | NexTek mRDT | 1 | 1 | 1 - limefaulu |
| 7 | Unigold HIV Test Kits | 2 | 2 | 2 - yamefaulu |
| 8 | Bioline mRDT | 5 | 5 | 5 - yamefaulu |
| **Jumla** | | **77** | **77** | **77** |

Matokeo ya uchunguzi wa kimaabara kwa matoleo 255 yameonesha kuwa bidhaa husika zimekidhi vigezo vya ubora na ufanisi.

### 2.2.4.2 Utekelezaji wa Mpango wa Ufuatiliaji wa Ubora na Ufanisi wa Vifaa Tiba na Vitendanishi *(PMS Programme)*

Mpango wa ufuatiliaji ubora na ufanisi wa vifaa tiba na vitendanishi (*PMS Programme*) ni mpango mahususi ulioandaliwa kwa vipindi vya miaka mitatu mitatu kwa lengo la kudhibiti bidhaa hizi katika soko baada ya kupata usajili na kuruhusiwa kuingia nchini kwa matumizi. Mpango huu unahusisha ukusanyaji wa sampuli, tathmini ya taarifa za lebo, uchunguzi wa maabara, uandaaji wa ripoti na kuchukua hatua za kiudhibiti.

#### (a) Ukusanyaji na Tathmini ya Taarifa Za Lebo

Katika kipindi cha mwaka 2024/2025 Sampuli 470 zilipangwa kukusanywa (vifaa tiba 345 na vitendanishi 125) za aina 10 ambazo ni *Blood Bags, HIV RDTs, I.V Giving Sets, Male Condoms, mRDTs, Sanitary Pads, Surgical Blades, Surgical Sutures, umbilical Cord Clamp na Urine Pregnancy Tests (UPT)* kama ilivyoainishwa katika mpango wa ufuatiliaji wa ubora na ufanisi wa vifaa tiba na vitendanishi wa miaka mitatu (2022/2023-2025/2026). Jumla ya sampuli 487 (Vifaa Tiba 369 na vitendanishi 118) sawa na 103.6% zimekusanywa katika mikoa nane (8) iliyopangwa katika Mpango. Tathmini ya taarifa za lebo (Product Information Review - PIR) ilifanyika ambapo sampuli 439 (vifaa tiba 346 na Vitendanishi 93) sawa na 90.1% zimefaulu *PIR* na sampuli 48 (vifaa tiba 23 na vitendanishi 25) sawa na 9.9% hazijafaulu tathmini kama ilivyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 34**.

**Jedwali Na. 34: Matokeo ya Ukusanyaji na Tathmini ya Taarifa za Lebo Sampuli za Mpango wa PMS 2024/25**

| Na. | Aina ya vifaa tiba na vitendanishi | Sampuli zilizopangwa kukusanywa | Sampuli zilizo-kusanywa | Kiwango cha ukusanyaji (%) | Zilizofanyiwa tathmini ya lebo | Zilizofaulu tathmini ya lebo | Zisizofaulu tathmini ya lebo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | UPT | 35 | 40 | 114.3 | 40 | 20(50%) | 20(50%) |
| 2 | mRDTs | 40 | 38 | 95.0 | 38 | 33(86.8%) | 5(13.2%) |
| 3 | HIV RDTs | 45 | 40 | 88.9 | 40 | 40(100%) | 0 |
| 4 | Surgical Sutures | 50 | 62 | 124.0 | 62 | 61(98.4%) | 1(1.6%) |
| 5 | Surgical Blades | 53 | 54 | 101.9 | 54 | 54(100%) | 0 |
| 6 | Sanitary Pads | 66 | 68 | 103.0 | 68 | 64(94.1%) | 4(5.9%) |
| 7 | IV Giving Sets | 63 | 62 | 98.4 | 62 | 62(100%) | 0 |
| 8 | Blood Bags | 17 | 20 | 117.6 | 20 | 20(100%) | 0 |
| 9 | Umbilical Cord Clamp | 80 | 80 | 100.0 | 80 | 62(90.1%) | 18(9.9%) |
| 10 | Male Condoms | 21 | 23 | 109.5 | 23 | 23(100%) | 0 |
| **Jumla** | | **470** | **487** | **103.6** | **487** | **439 (90.1)** | **48(9.7%)** |

**Ufunguo:** UPT – Urinary Pregnancy Test, mRDT – Malaria Rapid Diagnostic Test na HIV RDT – Human Immunodeficiency Virus Rapid Diagnostic Test

Kwa ujumla mapungufu yaliyoonekana kwenye lebo na taarifa za matumizi zinazoambatana na bidhaa ambapo nyingi zikiwa na ukosefu wa namba ya toleo, utofauti wa rangi kwenye lebo na maandishi kwa sampuli zilizoko katika soko kwa kulinganisha na zile zilizosajiliwa na uwepo wa matoleo tofauti ya vitendanishi yaliyochanganywa katika boksi moja.

### (b) Uchunguzi wa Maabara

Jumla ya sampuli 480 (98.6%) kati ya 487 zilizokusanywa ziliwasilishwa maabara kwa uchunguzi. Matokeo ya uchunguzi wa sampuli 301 (62.7%) yamepokelewa na kufuzu vigezo vya ubora na ufanisi katika vigezo vyote vilivyochunguzwa na uchunguzi bado unaendelea kwa sampuli zilizobaki. Mchanganuo wa matokeo ya uchunguzi wa maabara kwa sampuli zilizowasilishwa imeoneshwa katika **Jedwali Na. 35.**

**Jedwali Na. 35: Matokeo ya Uchunguzi wa Maabara**

| Na | Aina ya kifaa tiba/ kitendanishi | Zilizopelekwa kwa uchunguzi | Zilizochunguzwa | Hazijachunguzwa | Zilizofaulu uchunguzi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | UPT | 38 | 35 | 3 | 35 (100%) |
| 2 | mRDTs | 37 | 35 | 2 | 35 (100%) |
| 3 | HIV RDTs | 40 | 37 | 3 | 37 (100%) |
| 4 | Surgical Sutures | 61 | 33 | 28 | 33 (100%) |
| 5 | Surgical Blades | 54 | 34 | 20 | 34 (100%) |
| 6 | Sanitary Pads | 67 | 51 | 16 | 51 (100%) |
| 7 | IV Giving Sets | 62 | 11 | 51 | 11 (100%) |
| 8 | Blood Bags | 20 | 15 | 5 | 15 (100%) |
| 9 | Umbilical Cord Clamp | 80 | 33 | 47 | 33 (100%) |
| 10 | Male Condoms | 21 | 17 | 4 | 17 (100%) |
| | **Jumla** | **480** | **301** | **179** | **301 (100%)** |

### (c) Hatua za Kiudhibiti

Taarifa ya uchunguzi wa kimaabara zilizopokelewa katika kipindi hiki hakuna sampuli ambayo haikufaulu uchunguzi. Hatua za kiudhibiti zitakazo jumuisha sampuli zisizofaulu tathmini ya taarifa za lebo na uchunguzi wa kimaabara zitachuliwa baada ya kukamilika kwa uchunguzi.

## 2.2.4.3 Ufuatiliaji wa Matukio Yatokanayo na Matumizi Ya Vifaa Tiba Na Vitendanishi (Vigilance)

### (a) Tathmini ya Taarifa ya Matukio/Malalamiko Yatokanayo na Matumizi ya Vifaa Tiba na Vitendanishi

Jumla ya taarifa za matukio na madhara 250 yatokanayo na matumizi ya vifaa tiba na vitendanishi zilipangwa kupokelewa na kufanyiwa tathmini katika kipindi cha mwaka 2024/2025 na jumla ya taarifa 309 (123.6%) zimepokelewa ambapo taarifa 287 (92.9%) zimefanyiwa tathmini ukilinganisha na mwaka 2023/2024 ambapo taarifa 254 zilipokelewa na kufanyiwa tathmini, kutoka kwa watumiaji na vituo vya kutolea huduma za afya zilipokelewa.Taarifa za watengenezaji nje ya nchi, taarifa za hatua za marekebisho ya kiusalama ( Field safety report (FSCA), ufuatiliaji ubora na ufanisi wa vifaa tiba na vitendanishi katika soko (PMS Reports) toka kwa watengenezaji, taarifa za Usasishaji Usalama (Periodic Safety Update Reports - PSUR) zilipokelewa. Taarifa 377 zilipokelewa ambapo taarifa 354 zilifanyiwa tathmini na hatua za kiudhibiti zilichukuliwa kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na. 36**.

Jedwali Na. 36:Taarifa za Madhara, Matukio na Ufuatiliaji Vifaa Tiba Katika Soko

| Na | Aina ya taarifa | Zilizopokelewa | Zilizotathminiwa | Hatua za kiudhibiti zilizochukuliwa |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Taarifa za madhara na matukio kutoka kwa watumiaji binafsi na vituo vya kutolea huduma za afya | 309 | 287 | Watengenezaji walielekezwa kufanya uchunguzi wa matukio yanayojirudia / yaliyohisiwa kuhusisha aina 21 ya vifaa:<br>*ARI Digital BP Monitor, Vacutech K-EDTA collection tubes, Sidak UPT RDT, Clindiag Fa200 Chemical analyzer, Getein BHA-3000 Automatic haematology analyzer, URIT-560 Urine Analyzer, Keling delivery bed, Cady Blood EDTA Collection Tube, Trident Infusion Giving Set, New Type M YR-88 Medical oxygen regulator, Medismart Sterile latex Surgical Gloves, Zinc oxide plaster-Shanghai Channelmed, Sinnowa Hematology analyzer, Smpplene Monofilament Polypropylene suture, Smnylon Monofilament Suture, Polyglactin 910 Absorbable Suture, Isyringe Sterile Safety Syringe Auto-Disable, Revital infusion Giving Set, Revital Syringe, Advacare Umblical Cord, IV Cannula with wings.*<br>Kifaa tiba aina ya ***Omnipaque Contrast Media*** kimezuiwa kutumika na kuondolewa katika soko. Vituo vilivyotoa taarifa vimeelekezwa kuhakiki nyaraka za manunuzi toka wasambazaji. |
| 2. | Taarifa za madhara na matukio ya vifaa tiba na vitendanishi kutoka kwa watengenezaji | 24 | 24 | Hakuna hatua za kiudhibiti zilizochukuliwa. Matukio yalihusisha vitendanishi vya ARVHITECT BNP ***Reagent Kit*** na ***Allinity s System*** (immunoassay analyzers), ambapo mtengenezaji amefanya tathmini na marekebisho. |
| 3. | Taarifa 25 za hatua za marekebisho ya kiusalama (***FSCA Reports***) zilipangwa kukusanywa | 24 | 24 | Ufuatiliaji wa taarifa kwa matoleo ya vitendanishi yaliyoingizwa nchini umefanyika. |
| 4. | Taarifa za ufuatiliaji vifaa tiba na vitendanishi katika soko (***PMS Reports***) kutoka kwa watengenezaji | 4 | 4 | Hakuna hatua za kiudhibiti zilizochukuliwa Tathmini ya vitendanishi vya ***STANDARD™.Q HBsAg Test, STANDARD™Q HIV 1/2 Ab 3-Line Test*** na ***STANDARD™.Q Syphilis Ab Test*** zilionesha kukidhi vigezo vya ubora na ufanisi. |
| 5. | Taarifa za Usasishaji Usalama (Periodic Safety Update Reports – PSUR) za vitendanishi. | 7 | 7 | Tathmini imeonesha hakuna taarifa mpya za usalama zilizobainika katika vipindi vya ufuatiliaji wa vitendanishi vya aina ya Bioline mRDTs (Ag.P.f), HIV/Syphilis Duo RDTs, mRDTs (Ag.P.f/Pan, Dengue Duo RDTs, Syphilis 3.0 RDTs, HCV RDTs na HIV RDTs ½ 3.0 |
| | **Jumla ndogo** | **368** | **346** | |
| 6. | Taarifa za uchunguzi (CAPA) wa matukio ya vifaa tiba ziliwasilishwa na watengenezaji | 9 | 8 | Taarifa 7 zina hoja za kujibu. Taarifa moja ***Heuer surgical blade*** imekubaliwa. Mtengenezaji wa Kifaa tiba cha ***EDTA Vacutech blood collection tube***, ameelekezwa kufanya mafunzo kwa watumiaji na kurudisha lebo iliyoidhinishwa wakati wa usajili. |
| | **Jumla Kuu** | **377** | **354** | |

### (b) Uhamasishaji wa Watoa Huduma ya Afya Juu ya Utoaji Taarifa za Madhara na Matukio ya Vifaa Tiba na Vitendanishi

Jumla ya Wahudumu wa Afya 2000 walipangwa kupewa mafunzo ya kuhamasishwa juu ya utoaji taarifa za madhara na matukio yatokanayo na matumizi ya vifaa tiba na vitendanishi kwa kipindi cha mwaka 2024/2025 katika mikoa 10 ya Tanzania bara.

Jumla ya Wahudumu wa afya 787(39%) walipatiwa mafunzo na kuhamasishwa juu ya utoaji taarifa za madhara na matukio yatokanayo na matumizi ya vifaa tiba na vitendanishi katika mikoa mitano (5). Ukilinganisha na mwaka 2023/2024 ambapo uhamasishaji ulifanyika katika mikoa nane (8) jumla ya vituo 111 vya utoaji huduma za afya vya serikali na binafsi vilitembelewa na wahudumu 1966 walihamasishwa. Jumla ya fomu za rangi ya chungwa 4500 za kutolea taarifa za madhara na matukio yatokanayo na matumizi ya vifaa tiba na vitendanishi zilisambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya.

### (c) Usimamizi Saidizi (Supportive Supervision) wa Vituo vya Kutolea Taarifa za Madhara na Matukio Yatokanayo na Matumizi ya Vifaa Tiba na Vitendanishi

Usimamizi saidizi umefanyika kwa Waratibu (vigilance focal person) kutoka mikoa minne (4) ya Morogoro, Dodoma, Dar es Salaam na Pwani, ambapo waratibu wapatao 39 walipatiwa mafunzo yenye lengo la kuwawezesha kufuatilia na kutoa taarifa za matukio yatokanayo na matumizi ya vifaa tiba na vitendanishi.

## 2.2.4.4 Utekelezaji wa Mpango wa Ufuatiliaji Ubora na Ufanisi na Vifaa Tiba Vikubwa Katika Soko

Ufuatiliaji wa vifaa tiba vikubwa visivyofanya kazi umefanyika katika mikoa yote 26 kufuatia hoja za ukaguzi wa CAG na kubaini uwepo wa vifaa tiba vikubwa 2,809 visivyofanya kazi katika vituo 272 vya kutolea huduma za afya ikiwa 238 ni vituo vya serikali na 34 ni vituo binafsi. Kati ya vifaa hivyo, 1690 vinatakiwa kuondoshwa katika matumizi na kuteketezwa, ambapo vifaa 1,361 (80%) vilikutwa katika vituo vya kutolea huduma za afya vya serikali. Vifaa vilivyobaki 1,119 vinatakiwa kufanyiwa matengenezo na vingine kupatiwa vifaa ambata (reagents/ accessories) ili viendelee kutumika.

Aidha, Mpango wa pili wa ufuatiliaji ubora, usalama na ufanisi wa vifaa tiba vikubwa (Post Marketing Surveillance Program for Medical Equipment 2024/25 - 2026/27) na Andiko (Manuscript) la Mpango limeandaliwa.

## 2.2.4.5 Hali ya Soko la Vifaa Tiba na Vitendanishi Nchini

Hali ya soko ni ya kuridhisha kutokana na vifaa vingi kukidhi vigezo vya ubora. Tathmini inaonyesha kuwa vifaa vingi vilivyosajiliwa/tambuliwa vipo katika makundi yasiyo hatarishi yaani kundi A na B. Aidha, kazi ya ukaguzi kupitia ofisi za kanda imeendelea kufanyika ikiwa ni pamoja na kuviondoa katika soko vifaa tiba na vitendanishi ambavyo havina ubora. Hii inadhihirisha kwamba uhatarishi wa bidhaa zilizopo katika soko siyo mkubwa.

Vilevile mifumo ya ufuatiliaji wa ubora/usalama na ufanisi iliyowekwa na mamlaka inahakikisha watumiaji wanapata bidhaa zilizo bora, salama na zenye ufanisi na hivyo kulinda afya ya watumiaji na wananchi kwa ujumla wake. Hata hivyo pamoja na kuwa na mifumo iliyo thabiti, kumekwepo na vifaa vikubwa visivyofanya kazi au kutumika katika vituo vya kutolea huduma za afya kutokana na uwepo wa changamoto mbalimbali zinazohusisha vifaa vikubwa kutofanyiwa matengenezo kinga, ugezi(calibration), kututeketeza/kuondoshwa vifaa

visivyofaa au visivyofanya kazi katika vituo vya kutolea huduma za afya. Eneo hili linaendelea kufanyiwa kazi kwa ukaribu.

Vile vile vituo vya kutolea huduma za afya kununua vifaa tiba kutoka katika vyanzo visivyo rasmi na hivyo kusababisha uwepo wa vifaa tiba visivyosajiliwa na ambavyo usalama na ufanisi wake haujahakikiwa. Mamlaka inaendelea kufuatilia aina hizi za vifaa tiba ili kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria.

### 2.2.4.6 Kazi za Mradi wa Breedime

Katika kipindi hiki PMS Programme ya tathmini ya taarifa za lebo kwa vitendanishi vya vipimo vya malaria (mRDTs), ujauzito (UPTs) na virusi vya homa ya ini (Hepatitis B Ag tests) umefanyika kwa sampuli 170(60.7%) zilizokusanywa. Jumla ya sampuli 52 (30.6%) kati ya sampuli 170 zimefaulu tathmini ya taarifa za lebo na sampuli 118 (69.4%) hazikufaulu. Aidha jumla ya aina 28 (*4 za* MRDT, 14 za UPT RTDs na 10 za HBsAg RDTs) hazikufaulu kati ya aina 45 (12 za MRDT, 19 za UPT RTDs na 14 za HBsAg RDTs) zilizokusanywa.

Mapungufu yaliyobainika kwenye vitendanishi ambayo haikufaulu ni kukosekana kwa taarifa za mtengenezaji, jina la kifaa kwenye karatasi ya maelezo ya matumizi (Information for Use-IFU), lebo kwenye kasha la nje zilibandikwa kwa karatasi. Hatua za kiudhibiti zimechukuliwa kwenye mradi wa BREEDIME kwa bidhaa aina 20 za vitendanishi visivyofaulu tathmini ya lebo ambapo watengenezaji wameelekezwa kufanya maboresho ya taarifa husika.

Taarifa za uchunguzi wa kimaabara zilizopokelewa katika kipindi hiki zimethibitisha kuwa hakuna sampuli ambayo haikufaulu uchunguzi. Hatua za kiudhibiti zitakazo jumuisha sampuli zisizofaulu tathmini ya taarifa za lebo na uchunguzi wa kimaabara zitachuliwa baada ya kukamilika kwa uchunguzi.

### 2.2.4.7 Kuandaa Mwongozo wa *Perfomance Evaluation na Protocols*

Kurugenzi imeandaa Mwongozo wa jinsi ya kufanya *Perfomance Evaluation* ya vitendanishi pamoja na *protocols* sita (6) kwa ajili ya kuwaelekeza wateja taratibu za kufuata wakati wa kupima ufanisi wa vitendanishi kupitia mradi wa Breedime. Mwongozo huo na *protocols* ni kama zilivyoainishwa hapa chini;

(a) Guidelines for Conducting Performance Evaluation of In-Vitro Diagnostic Devices Submitted for Marketing Authorization, June, 2024

(b) Protocol for Performance Laboratory Evaluation of Malaria Plasmodium Falciparum (PF) and MALARIA PF/PAN Antigen Rapid Diagnostic Tests, First Edition, April, 2024

(c) Protocol for Performance Laboratory Evaluation of Combined HIV and Syphilis Serology Assays, First Edition, April, 2024

(d) Protocol for Performance Laboratory Evaluation of HIV Serology Assays, First Edition, April, 2024

(e) Protocol for Performance Laboratory Evaluation of Hepatitis C Serology Assays, First Edition, April, 2024

(f) Protocol for Laboratory Performance Evaluation of Hepatitis B Surface Antigen, First Edition April 2024

(g) Protocol for Laboratory Performance Evaluation of SARS-CoV-2 Antigen Assays, First Edition April 2024

### 2.2.4.8 Kupitia "Performance Evaluation Data" Katika Maombi ya Usajili wa Vitendanishi

Mamlaka ilifanya mapitio ya violezo vinavyotumika kufanya tathmini ya vitendanishi katika eneo la "perfornance evaluation" na tathmini ya vifaa tiba vyenye uhatarishi mkubwa katika eneo la "clinical evidence". Vile vile maombi ya usajili wa vifaa tiba na vitendanishi 34 yalipitiwa ili kuhakiki kama tarifa zilizoletwa zilifuata utaratibu uliohusishwa katika "protocols" zilizotengenezwa. Hata hivyo ripoti za tathmini zilionesha mapungufu kadhaa ambayo yalishawasilishwa kwa wateja kipindi cha tathmini. Hivyo, ili kuboresha eneo hili, Kurugenzi inaendelea kufanya vikao na wadau ili waweze kuelewa na kufuata taratibu zilizoainishwa katika miongozo.

### 2.2.4.9 Uteketezaji wa Bidhaa Zisizokidhi Viwango

Mamlaka huteketeza bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi ambazo hazikidhi vigezo vya ubora, usalama na ufanisi ili kuepusha bidhaa husika zisitumiwe na watumiaji. Bidhaa zinazoteketezwa zinajumuisha zile zinazoombewa kibali (voluntary disposal) na wateja wenyewe kutokana na kuisha muda wa matumizi na zilizokamatwa katika kaguzi mbalimbali kwa sababu hazijasajiliwa, kuwa duni na bandia baada ya uchunguzi wa kimaabara au zinazokutwa kwenye maeneo ambayo hayajasajiliwa. Uzito na thamani za bidhaa zilizoteketezwa katika kipindi hiki umeainishwa katika **Jedwali Na. 37**

**Jedwali Na. 37: Mchanganuo wa Bidhaa Zisizo na Ubora Zilizoteketezwa**

| Na | Aina ya bidhaa | Mchanganuo | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Vilivyotolewa taarifa | | Vilivyokamatwa | |
| | | Uzito (Tani) | Thamani (TZS) | Uzito (Tani) | Thamani (TZS) |
| 1 | Dawa za binadamu | 358.50 | 8,106,295,168.38 | 4.01 | 209,382,704.00 |
| 2 | Dawa za mifugo | - | - | 1.85 | 163,254,221.00 |
| 3 | Vifaa tiba | 287.09 | 1,876,253,507.02 | 2.84 | 52,819,360.00 |
| 4 | Vitendanishi | 0.02 | 2,112,750.00 | | |
| **Jumla** | | **645.62** | **9,984,661,425.40** | **8.70** | **425,456,285.00** |

Kwa mujibu wa **Jedwali Na. 37** hapo juu, jumla ya tani 654.32 (tani 645.62 zilizotolewa taarifa na tani 8.7 zilizokamatwa) za bidhaa zenye thamani ya takriban TZS 10.41 bilioni ziliteketezwa kutokana na kutokukidhi vigezo vya ubora na usalama. Kiasi cha bidhaa zilizoteketezwa ni ongezeko tani 326.73 ukilinganisha na tani 327.59 zilizoteketezwa katika kipindi kama hiki mwaka 2023/24.Ongezeko hili limechangiwa na bidhaa zinazotolewa taarifa na wafanyabiashara.



## 2.3.0 KUIMARISHA UDHIBITI WA BIDHAA ZA TUMBAKU

Kwa kutambua madhara yanayosababishwa na matumizi ya bidhaa za Tumbaku, Mamlaka imepewa jukumu la kusimamia bidhaa hizi. Kazi zilizotekelezwa katika kipindi hiki ni kukagua maeneo yanayojihusisha na uendeshaji wa biashara ya bidhaa za tumbaku ikiwa ni pamoja na maduka, maghala ya kuhifadhi bidhaa za tumbaku pamoja na maeneo ya umma yanayohusika na bidhaa hizi. Mchanganuo wa ukaguzi wa maeneo ya biashara za bidhaa za tumbaku umeainishwa na **Jedwali Na. 38.**

**Jedwali Na. 38: Ukaguzi wa Maeneo ya Biashara za Bidhaa za Tumbaku**

| Na. | Aina ya Biashara | Yaliyopangwa kukaguliwa | Yaliyokaguliwa | Yaliyokidhi Vigezo | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Idadi | % |
| 1. | Maduka ya Jumla | 25 | 74 | 35 | 47 |
| 2. | Maduka ya rejareja | 292 | 387 | 333 | 86 |
| 3. | Maghala | 7 | 4 | 4 | 100 |
| 4. | Maeneo ya Umma (Bar/Supermarket) | 220 | 536 | 207 | 39 |
| **Jumla Kuu** | | **544** | **1001** | **579** | **58** |

Kwa mujibu wa **Jedwali Na. 38** jumla ya maeneo 1001 sawa na 184% ya maeneo yaliyopangwa yalikaguliwa. Maeneo 579 (58%) yaliyokaguliwa yalikidhi vigezo. Maeneo yaliyokaguliwa katika kipindi hiki ni ongezeko la maeneo 569 (131%) ukilinganisha na maeneo 432 yaliyokaguliwa mwaka 2023/24.



# 3.0 KUBORESHA HUDUMA ZA MAABARA

Katika kipindi hiki Mamlaka ilitekeleza majukumu ya maabara ikiwa ni pamoja na uchunguzi wa sampuli za dawa, vifaa tiba na vitendanishi pamoja na kufanya utafiti kuhusu ubora na usalama wa bidhaa kama ilivyoainishwa kwenye kipengele **Na. 3.1 – 3.7** na **Majedwali 39 hadi 42**.

## 3.1 Uchunguzi wa Sampuli za Bidhaa Zinazodhibitiwa

Jumla ya sampuli 1,940 za dawa, vifaa tiba, vitendanishi na vipukusi zilipokelewa, ambapo sampuli 1,394 zilipokelewa katika Maabara ya Dar es salaam na sampuli 546 zilipokelewa katika Maabara ya Mwanza. Vilevile, kulikuwa na sampuli tano (5) ambazo ni baki kutoka mwaka 2023/2024. Hivyo kufanya jumla ya sampuli kuwa 1,945. Sampuli 1,820 sawa na 93.6% zilifanyiwa uchunguzi ambapo sampuli 1,694 (93.1%) zilifaulu.

## 3.2 Uchunguzi wa Sampuli za Dawa Dar es salaam

Kulikuwa na jumla ya sampuli 575 za dawa zilizopaswa kuchunguzwa ambapo sampuli 570 kati ya hizo zilipokelewa katika kipindi cha Julai 2024 – 31 Juni 2025 na sampuli 5 zilikuwa baki kutoka mwaka 2023-2024 wa fedha. Sampuli 572 (99.5%) zilichunguzwa ambapo sampuli 551 (96.3%) zilifaulu kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 39**

**Jedwali Na. 39: Uchunguzi wa Sampuli za Dawa**

| Chanzo cha sampuli | Baki (2023-24) | Pokelewa | Jumla | Chunguzwa | Baki | Faulu | % Faulu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ukaguzi-binadamu | 1 | 28 | 29 | 29 | 0 | 19 | 65.5 |
| Usajili | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Sampuli za utafiti (Miscellaneous)* | 0 | 225 | 225 | 225 | 0 | 224 | 99.6 |
| Wateja wa nje-binadamu | 2 | 59 | 61 | 60 | 1 | 50 | 83.3 |
| Ufuatiliaji wa bidhaa sokoni (PMS) | 2 | 258 | 260 | 258 | 2 | 258 | 100 |
| **Jumla** | **5** | **570** | **575** | **572** | **3** | **551** | **96.3** |



## 3.3 Uchunguzi za Sampuli za Vifaa Tiba na Vitendanishi

Katika kipindi husika Mamlaka ilipokea jumla ya sampuli 824 (vifaa tiba 620 na vitendanishi 204) na hakukuwa na sampuli baki kutoka mwaka jana wa fedha. Sampuli 702 (85.1%) zilichunguzwa ambapo sampuli 603 (85.9%) zilifaulu kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 40**.

Jedwali Na. 40: Uchunguzi wa Sampuli za vifaa tiba na Vitendanishi

| Bidhaa | Chanzo cha Sampuli | Baki 2023-24 | Pokelewa | Jumla | Chunguzwa | Baki | Faulu | % Faulu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Vifaa tiba | Ukaguzi | 0 | 175 | 175 | 175 | 0 | 175 | 100 |
| | Ufuatiliaji wa bidhaa sokoni (PMS) | 0 | 345 | 345 | 223 | 122 | 126 | 100 |
| | Uchunguzi wa utafiti | 0 | 38 | 38 | 38 | 0 | 36 | 94.7 |
| | Wateja wa nje | 0 | 62 | 62 | 62 | 0 | 62 | 100 |
| | **Jumla ndogo** | **0** | **620** | **620** | **498** | **122** | **399** | **80.1** |
| Vitendanishi | Wateja wa nje | 0 | 2 | 2 | 2 | 0 | 2 | 100 |
| | Ufuatiliaji wa bidhaa sokoni (PMS) | 0 | 134 | 134 | 134 | 0 | 134 | 100 |
| | Ukaguzi | 0 | 68 | 68 | 68 | 0 | 68 | 100 |
| | **Jumla ndogo** | **0** | **204** | **204** | **204** | **0** | **204** | **100** |
| **Jumla kuu** | | **0** | **824** | **824** | **702** | **122** | **603** | **85.9** |

**% Faulu ya uchunguzi wa Sampuli za vifaa tiba**




**% Faulu ya uchunguzi wa Sampuli za vitendanishi**





## 3.4 Uchunguzi wa Sampuli za Dawa na Vipukusi Mwanza

Katika kipindi husika Maabara ya Mwanza ilipokea jumla ya sampuli **546** (dawa 479, na 67 vipukusi), na hakukuwa na sampuli baki kutoka mwaka jana wa fedha. Sampuli zote 546 (100%) zilichunguzwa ambapo sampuli 540 (98.9%) zilifaulu kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na.41.**

**Jedwali Na. 41: Uchunguzi wa Sampuli za Dawa na Vipukusi**

| Bidhaa | Chanzo cha Sampuli za Bidhaa | Baki | Pokelewa | Jumla | Chunguzwa | Baki | Faulu | % Faulu |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Dawa | Ufuatiliaji Sokoni (PMS) | 0 | 236 | 236 | 236 | 0 | 236 | 100 |
| | Uchunguzi wa awali | 0 | 243 | 243 | 243 | 0 | 243 | 100 |
| | Wateja wa nje | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | **Jumla Ndogo** | **0** | **479** | **479** | **479** | **0** | **479** | **100** |
| Vipukusi | Ufuatiliaji Sokoni (PMS) | 0 | 67 | 67 | 67 | 0 | 61 | 91 |
| | **Jumla Ndogo** | **0** | **67** | **67** | **67** | **0** | **61** | **91** |
| **Jumla Kuu** | | **0** | **546** | **546** | **546** | **0** | **540** | **99** |

## 3.5 Uchunguzi wa Awali wa Dawa Katika Maabara Hamishika

Jumla ya sampuli za dawa 3861 zimefanyiwa uchunguzi wa awali kwa kutumia maabara hamishika katika vituo vyote 27 kuanzia Julai 2024 hadi Juni 2025. Sampuli zote 3861 zilizochunguzwa, zilifaulu vipimo vya uchunguzi kama inavyoonekana katika **jedwali Na. 42.**

**Jedwali Na. 42: Vituo vya Maabara Hamishika**

| Na. | KANDA | KITUO | CHUNGUZWA | IDADI ILIYOPANGWA (MWAKA) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kanda ya Ziwa Magharibi | 1. TMDA WLZ | 30 | 100 |
| | | 2. Bukoba RRH | 206 | |
| | | 3. Mtukula – POE | 69 | |
| | | **Jumla ndogo** | **305** | |
| 2 | Kanda ya Ziwa Mashariki | 4. Musoma RRH | 197 | 500 |
| | | 5. Sirari - POE | 62 | |
| | | 6. Simiyu RRH | 154 | |
| | | **Jumla ndogo** | **413** | |
| 3 | Kanda ya Kaskazini | 7. Manyara RRH | 42 | 240 |
| | | 8. Kilimanjaro RRH | 432 | |
| | | 9. Tarakea POE | 52 | |
| | | 10. Namanga – POE | 141 | |
| | | 11. NZ -TMDA | 166 | |
| | | **Jumla ndogo** | **833** | |
| 4 | Kanda ya Mashariki | 12. Horohoro – POE | 38 | 1100 |
| | | 13. Bombo RRH | 69 | |
| | | 14. EZ - TMDA | 376 | |
| | | **Jumla ndogo** | **483** | |
| 5 | Kanda ya Kusini | 15. Lindi RRH | 123 | 200 |
| | | 16. Mtwara RRH | 67 | |
| | | 17. Songea RRH | 198 | |
| | | **Jumla ndogo** | **388** | |
| 6 | Kanda ya Nyanda za Juu Kusini | 18. Mbeya RRH | 396 | 200 |
| | | 19. Tunduma – POE | 340 | |
| | | 20. Sumbawanga RRH | 189 | |
| | | **Jumla ndogo** | **925** | |
| 7 | Kanda ya Kati | 21. Iringa RRH | 137 | 200 |
| | | 22. Dododoma – TMDA | 74 | |
| | | 23. Morogoro RRH | 35 | |
| | | 24. Singida RRH | 52 | |
| | | **Jumla ndogo** | **298** | |
| 8 | Kanda ya Magharibi | 25. WZ - TMDA | 42 | 200 |
| | | 26. Kigoma RRH | 92 | |
| | | 27. Katavi RRH | 76 | |
| | | **Jumla ndogo** | **210** | |
| | | **Jumla Kuu** | **3861** | **2740** |


TRUSTED FOR OUR STANDARDS

IAF INTERNATIONAL ACCREDITATION FORUM

ACM CERTIFICATION

ACM

Certificate of Registration

This is to certify that the
Quality Management System
of

**Tanzania Medicines and Medical Devices Authority**
Mabibo External
P.O Box 77150
Dar es Salaam
Tanzania

Has been independently assessed and is
compliant with the requirements of:

ISO 9001:2015

## 3.6 Utekelezaji wa Mifumo ya Ubora wa Utendaji Kazi (ISO/IEC 17025:2017 na WHO/GPPQCL)

Mamlaka iliendelea kutekeleza matakwa ya kiwango cha ISO/IEC 17025:2017 kwa uchunguzi wa Vifaa Tiba na Vitendanishi, pamoja na Mwongozo wa Shirika la Afya Duniani (WHO) wa Utambuzi wa Umahiri wa Maabara (WHO Prequalification) kwa upande wa uchunguzi wa dawa. Aidha, mpaka sasa maandalizi ya kufikia viwango vya shirika la Afya Duniani (WHO) katika uchunguzi wa dawa kwa maabara ya Mwanza imefikia 80% kwa

- Uhuishaji wa *Quality Manual*, *Standard operating procedures*
- Kufanya mafunzo kwa watumishi kuhusiana na SOPs na njia za kiuchunguz
- Kuhakikisha mashine zote za uchunguzi zimefanyiwa ugezi na matengenezo kinga;
- Kutunza nyaraka za kazi za maabara katika maeneo stahiki;
- Kuchagua na kuhakiki njia za uchunguzi zitakazoombewa Ithibati; na
- Kuainisha vihatarishi katika taratibu zinazohusiana na uchunguzi wa sampuli na kuvipangia mpango kazi wa kuviondoa.

## 3.7 Ugezi, Matengenezo na Ununuzi wa Vifaa, Kemikali na Mahitaji Mengine ya Maabara

Mamlaka ilipokea baadhi ya kemikali, kemikali rejea na vifaa mbalimbali (*consumables)* za maabara kutoka kwa wazabuni. Pia imefanya ugezi, matengenezo dharura na kinga kwa vifaa vya maabara ya Dodoma, Mwanza na Dar es salaam ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mpango kazi na bajeti.

# 4.0 KUIMARISHA UTOAJI ELIMU KWA UMMA NA KUBORESHA HUDUMA KWA WATEJA

Mamlaka ililenga kuimarisha utoaji wa elimu kwa umma na huduma kwa wateja ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata taarifa sahihi juu ya kazi na majukumu yake sanjari na kujengewa uelewa wa taratibu za kuanzisha biashara ya dawa za binadamu na mifugo pamoja na vifaa tiba. Kipengele **4.1- 4.2** kimeainisha namna Mamlaka ilivyotekeleza lengo hili kwa kipindi cha Julai, 2024 – Juni, 2025.

## 4.1 Utoaji Elimu kwa Umma

Elimu kwa umma husaidia kuongeza uelewa kwa watumiaji wa bidhaa zinazodhibitiwa na Mamlaka na wananchi kwa ujumla na hivyo kusaidia matumizi sahihi ya bidhaa pamoja na kuongeza utii wa Sheria bila shuruti. Kazi za uelimishaji umma zilizotekelezwa katika kipindi hiki ni kama zilivyoorodheshwa katika **Jedwali Na 43.**

**Jedwali Na. 43: Njia Zilizotumika Kuelimisha Jamii**

| Na. | Kazi zilizofanyika | Lengo | Idadi iliyofikiwa | Maelezo/Maoni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mihadhara ya wazi kwa Umma | 200 | 267 | Kufanya mihadhara kwa vikundi vya uzalishaji vya vijana wanawake na wananchi pamoja na waalimu na wanafunzi katika shule za sekondari na vyuo katika mikoa ya Manyara, Tanga, Kigoma, Katavi, Dodoma, Iringa, Tabora, Geita, Dodoma, Kagera Mtwara, Lindi, Arusha, Morogoro, Kilimanjaro, Rukwa, Singida na Njombe ambapo jumla ya washiriki 115,129 walifikiwa |
| 2. | Ushiriki wa maonesho | 10 | 13 | Kushiriki katika maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es salaam (Sabasaba) na Maonesho ya wakulima (Nanenane), maonesho ya Kimataifa ya Africa, maonesho ya Wajasiriamali wadogo Afrika Mashariki (Jua Kali Nguvu Kazi), wiki ya Famasi na Mkutano mkuu wa Chama cha Wafamasia Tanzania (PST) maonesho ya Biashara ya Afrika Mashariki Jijini Mwanza, (maonesho) Maonesho ya Viwanda vya Tanzania (TIMEXPO 2024) na maonesho ya wiki ya Sheria |
| 3. | Urushaji wa vipindi katika Radio na Runinga | 100 | 102 | Vipindi vya moja kwa moja kuhusu matumizi sahihi ya dawa vilirushwa kupitia radio za kijamii na kibiashara nchini ikiwemo; AZAM TV, ITV, Clouds TV, Tumaini TV na TBC, Newala FM, Selous FM, Bunda FM, Mazingira FM, Sibuka FM, Bariadi FM, U FM, Radio Tumaini, Clouds FM, Wasafi FM, Radio Maria, Newala FM, Selous FM, Chai FM, Rungwe FM, Keifo FM, Kyela FM, Kitulo FM, Green FM, Kings FM, Uplands FM, Ludewa FM, Pambazuko FM, Singida Blogu, Radio Safina, Redio Habari Maalumu Arusha, Radio five, Radio Shalom FM, Jambo TV na Nyota FM. |

| Na. | Kazi zilizofanyika | Lengo | Idadi iliyofikiwa | Maelezo/Maoni |
|---|---|---|---|---|
| 4. | Kuandaa na kusambaza vielelezo vya uelimishaji umma | 25 | 22 | Kuandaa Makala (documentary) kuhusu mradi wa PAVIA, T-Shirt, jarida la TMDA Toleo la 14 Mashati ya watumishi, vipeperushi vya maabara, kalenda na shajara za mwaka 2025, vikombe, vipeperushi, kitabu kuhusu Historia ya Baraza, notebook, mabango, trophies, kalamu na mifuko ya kuitangaza Mamlaka. |
| 5. | Kutoa taarifa na matangazo kwa umma | 50 | 66 | Taarifa kwa umma 36 kuhusu kazi na majukumu ya TMDA zilitolewa kupitia tovuti, magazeti na mitandao ya kijamii. Matangazo yalihusu usalama wa dawa ya paracetamol, usomaji wa taarifa ya mwisho wa matumizi katika dawa, Maadhimisho ya wiki ya Wafamasia, Matumizi ya dawa za ARV kunenepesha mifugo, Ofisi ya Kanda ya Kusini kuhamia Ruvuma, Tahadhari za ugonjwa wa Mpox, maadhimisho ya sherehe za Nanenane na Eid. Vilevile kumbukizi ya Uhuru, Kifo cha Baba wa Taifa, salamu za pole kufuatia kifo cha Mhe. Dkt. Faustin Ndugulile na salamu za Krismasi |
| 6. | Kupandisha taarifa kwenye tovuti ya TMDA. | 500 | 537 | Taarifa zilizopandishwa katika tovuti zinajumuisha picha, taarifa kwa umma, machapisho na taarifa za kanda |
| 7. | Kupandisha taarifa kwenye kurasa za mitandao ya kijamii za TMDA. | 2,000 | 1,434 | Taarifa zimepandishwa katika kurasa za mitandao ya kijamii ya facebook, twitter, instagram na youtube ambapo chapisho la taarifa ya tangazo kwa umma kuhusu kikao cha pamoja kwa watengenezaji na wabunifu wa ndani wa vifaa tiba na vitendanishi pamoja na chapisho la picha mjongeo ya Mhe. Rais Dkt. Samia akihutubia Baraza la Afya Duniani, yalionwa na zaidi ya watu 11,178. |
| 8. | Kufanya mikutano na waandishi wa habari. | 1 | 1 | Mkutano na Wahariri na Waandishi Kanda ya Ziwa Magharibi umefanyika Tabora. |
| 9 | Klabu za Shule | 50 | 73 | Klabu 130 za TMDA zilianzishwa katika shule za sekondari zilizopo katika mikoa ya Dar es salaam, Pwani, Arusha, Katavi, Kigoma, Mara, Mwanza, Mbeya, Singida na Rukwa. |

## 4.2 Kuboresha Huduma kwa Wateja

Katika kuhakikisha kuwa utoaji wa huduma kwa wateja ni wa kiwango bora, Mamlaka ilitekeleza kazi mbalimbali kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali Na. 44.**

**Jedwali Na. 44: Kazi za Kuboresha Huduma kwa Wateja**

| Na. | Kazi zilizofanyika | Idadi iliyofikiwa | Maelezo/Maoni |
|---|---|---|---|
| 1. | Utoaji wa Huduma kwa wateja | 13,132 | Wateja walihudumiwa kupitia dawati la huduma kwa wateja na maktaba ambapo walipatiwa huduma stahiki |
| 2. | Hoja za wateja zilizopokelewa | 20 | Hoja 20 kuhusu usalama wa dawa na vifaa tiba katika soko zilipokelewa na kufanyiwa kazi ambapo hoja zote zimekamilika |
| 3. | Hoja za wateja zilizofanyiwa kazi na kukamilika | | |
| 4. | Kuhamasisha wadau kuhusu utoaji wa taarifa za udokezi | 106,167 | Wananchi na wadau 106,167 walihamasishwa kuhusu será ya udokezi ambapo uhamasishaji ulifanyika sambamba na zoezi la utoaji elimu kwa njia ya mihadhara ambapo sera ya udokezi ilikuwa ni moja ya mada. |
| 5. | Wafuatiliaji wa mitandao ya kijamii ya TMDA | 383,940 | Idadi ya wafuasi (followers) katika mitandao ya kijamii imeongezeka kufikia 24,500 instagram, 16,302 facebook, 343,000 X na 140 youtube |

Aidha, kazi zifuatazo zilifanyika katika kipindi hiki kwa lengo la kuboresha huduma kwa wateja:-

- Kupokea na kufanyia kazi taarifa 1 ya udokezi ambapo pia mrejesho ulitolewa kwa mdokezi;
- Kufanya tathimini ya kiwango cha wadau kuridhika na huduma za TMDA (SDS) kwa kushirikiana na Wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; na
- Kuhamasisha watumishi 41 kuhusu utoaji huduma kwa wateja kwa kuzingatia maadili ya utumishi wa umma.
- Vile vile, wateja 512 walishiriki katika zoezi la kutoa maoni baada ya kupokea huduma ambapo wateja 486 walithibitisha kuridhika na kiwango cha huduma sawa 94.9% ya wateja wote huku wateja 26 wakihitaji maboresho zaidi kwenye huduma waliyopatiwa.

# 5.0 KUIMARISHA UWEZO WA TAASISI KUTOA HUDUMA ZA UDHIBITI

Mamlaka haina budi kuimarisha uwezo wake kwa kuwa na vitendea kazi mbalimbali ikiwemo majengo ya ofisi na maabara, magari, vifaa vya TEHAMA, kuongeza idadi ya watumishi na kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ili kugharamia shughuli zote za udhibiti kwa mujibu wa Sheria. Katika kipindi cha mwaka 2024/25, kazi mbalimbali zilitekelezwa chini ya lengo Mkakati hili kama zilivyoainishwa katika kipengele **5.1 – 5.9**

## 5.1 Usimamizi wa Rasilimali Watu

Katika kipindi cha Julai 2024 - Juni 2025, masuala yaliyofanyiwa kazi ni pamoja na kukamilisha ajira mpya, mafunzo na kujiendeleza katika kazi, usimamizi wa ustawi wa watumishi na michezo. Aidha, Mamlaka imeendelea kusimamia utekelezaji wa mfumo wa Usimamizi wa Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma (PEPMIS), kulipa stahili na motisha mbalimbali za watumishi na usimamizi wa masuala ya uadilifu na utawala bora ndani ya Taasisi.

### 5.1.1 Idadi Ya Watumishi

Hadi kufikia mwezi Juni 2025 TMDA ilikuwa na jumla ya watumishi 430 wa ajira ya kudumu na malipo ya pensheni. Idadi hii ni ongezeko la watumishi 110 ikilinganishwa na idadi ya watumishi 320 waliokuwepo mwezi Juni, 2024. Hata hivyo, idadi hii ya watumishi wanaotekeleza majukumu ya Mamlaka katika Ofisi ya Makao Makuu, Kanda na katika vituo vya forodha ni ndogo ukilinganisha na idadi ya watumishi 488 wanaostahili kuwepo kulingana na Mpango wa Rasilimaliwatu wa Mamlaka 2025.

### 5.1.2 Utekelezaji Wa Mfumo Wa Usimamizi Wa Utendaji Kazi Katika Utumishi Wa Umma

Mamlaka imeendelea kutekeleza Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma (PEPMIS) na Mfumo wa Upimaji Utendaji Kazi wa Taasisi (PIPMIS). Katika mwaka wa fedha ulioanza Julai 2024 watumishi wote waliingiza majukumu waliyopangiwa kwa mwaka 2024/25 ndani ya mfumo na kuwekewa vigezo vyote stahili na wasimamizi wao wa kazi.

Aidha, hatua ya utekelezaji na ufuatiliaji (Implementation and Monitoring) inaendelea pamoja na maboresho kwenye baadhi ya kazi kwa watumishi wanaohamia au waliobadilishiwa majukumu. Hadi kufikia mwezi Juni 2025, Mamlaka ilikuwa imefikia 81.7% za utekelezaji kwenye Mfumo wa PEPMIS ambayo inaenda sambamba na utekelezaji kwenye Mfumo wa PIPMIS.

### 5.1.3 Mafunzo kwa vitendo

TMDA kama Taasisi ya Umma inapokea wanafunzi wa sekta ya afya kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo. Katika kipindi hiki, Mamlaka ilipokea Wafamasia Watarajali (Intern Pharmacists) 27 waliopangwa na Wizara ya Afya kuja TMDA. Aidha, Mamlaka hupokea wanafunzi wa vitendo (field students) kutoka vyuo mbalimbali kwa ajili ya kupata mafunzo kwa nyakati tofauti katika Kurugenzi, Vitengo na Ofisi za Kanda.

### 5.1.4 Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini.

Katika kutekeleza Sheria ya Afya na Usalama Kazini Na. 5 ya mwaka 2003 na Kanuni mbalimbali zinazohusiana na Sheria hii, Mamlaka imenunua viti maalum vya migongo 55, meza 46, viti vya kantini 36, meza za kantini 18. Pia, Menejimenti inaendelea na kuhimiza utamaduni wa watumishi kusimama hasa wanapokuwa wanahudhuria vikao au kutekeleza majukumu ndani ya ofisi zao.

### 5.1.5 Ushiriki wa Michezo Kwa Watumishi

Mamlaka katika kutekeleza malengo yake, imeweka kipaumbele cha kuhakikisha watumishi wanashiriki michezo mbalimbali kwa lengo la kuimarisha afya ya mwili na akili ikiwa ni pamoja na kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza. Katika kipindi hiki Mamlaka imeendelea kuhamasisha watumishi kufanya mazoezi mbalimbali. Aidha Mamlaka imeshiriki katika mashindano ya Taasisi za Serikali zilizopo mkoani Dar es Salaam kwa jina la *Dar es salaam Staff Sports League* (*DSSL)* ambayo yamehitimishwa mwezi Juni 2025.

### 5.1.6 Taarifa ya Utendaji wa Kamati Mbalimbali

#### (a) Kamati Ya Uadilifu

Mamlaka ina Kamati ya Uadilifu ambayo inatekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Mkakati wa Taifa dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji awamu ya nne ya (NACSAP IV) 2023-2030. Katika kipindi hiki, Kamati haijapokea taarifa/ tukio kuhusu changamoto ya masuala ya uadilifu.

#### (b) Kamati ya Ajira

Kamati ya Ajira ilikutana na kufanya kikao chake tarehe 12 Juni, 2025.Masuala yaliyojadiliwa ni pamoja na watumishi 42 wanaostahili kuthibitishwa kazini, bajeti ya Mishahara na Ikama ya watumishi kwa mwaka 2025/26 pamoja na utekelezaji wa Kibali cha Ajira cha nafasi 55. Watumishi 53 wamepokelewa na kupangiwa vituo vya kazi kutokana na idhini ya Kibali tajwa.

Pia, Mamlaka imepokea kibali cha utekelezaji wa Ikama kwa Mwaka 2024/2025 ambapo Kibali cha ajira nafasi 35, kupandisha vyeo watumishi 51 na kubadilishwa kada watumishi nane (8) wenye sifa. Taratibu za kuwaingiza kwenye mfumo wa e - Watumishi unaendelea ili kupata idhini ya mabadiliko ya mishahara.

### 5.1.7 Maboresho ya Muundo wa Maendeleo ya Watumishi na Muundo wa Mishahara

Mamlaka imewasilisha ombi la idhini ya maboresho ya Muundo wa Maendeleo ya Utumishi kwa watumishi wa TMDA (Scheme of Service) na Muundo wa Mishahara (Salary structure), mapendekezo ambayo yalipitishwa na Menejimenti, Chama cha Wafanyakazi TUGHE tawi la TMDA na Bodi ya Ushauri (MAB) na kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu Utumishi kwa kibali. Taratibu za mawasiliano na ufuatiliaji zinaendelea katika ofisi ya Katibu Mkuu, Ofisi ya Raisi Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Msajili wa Hazina.

### 5.1.8 Uhakiki Mifumo na Usimamizi wa Vihatarishi

Mamlaka imetekeleza kazi za uhakiki mifumo na usimamizi wa vihatarishi kama ifuatavyo: -

(a) Kuandaa, kufanyia mapitio na kusambaza kwa watumiaji nyaraka 231 zikiwemo; Taratibu Sanifu za Utendaji kazi (SOPs) 72, fomu 76, michakato (process flows) 43, checklists 10, rejesta 17, mipango minne (4) na miongozo sita (6) kusaidia utekelezaji wa majukumu. Sambamba na kazi hiyo, jumla ya nyaraka 781 zilizopo kwenye mifumo ya kielektroniki ya ***Intranet*** na ***RIMS*** zilifanyiwa uhakiki ili kuhakikisha kuwa watumiaji wanapata toleo sahihi la nyaraka wakati wowote, kwa urahisi na kwa ufanisi.

(b) Kufanya tathmini ya michakato miwili (2) ya mfumo wa uhakiki ubora wa huduma. Maeneo ya maboresho yaliyoainishwa katika taarifa ya tathmini ya michakato yaliwasilishwa kwa wahusika kwa utekelezaji.

(c) Kutekeleza mpango wa kutibu vihatarishi 92 vinavyoweza kuathiri kufikiwa kwa malengo mkakati ya taasisi (***institutional risks***), mpango wa kutibu vihatarishi vya udanganyifu 59 vinavyoweza kuathiri rasilimali za taasisi ikiwemo mwenendo wa kukusanya mapato na matumizi yake (***fraud risks***), na mpango wa kutibu vihatarishi vinavyoweza kuathiri utekelezaji wa michakato ya kazi (***process objective risks***) kufikia malengo madogo (***targets***) kwa upande wa Kurugenzi ya DBS, Kurugenzi ya DMD, Kurugenzi ya DMC na Vitengo vilivyopo chini ya Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu.

(d) Kufanya uchambuzi wa vihatarishi vipya vinavyoweza kuathiri utekelezaji wa majukumu (***process risks***) pamoja na kuandaa mpango kazi wa kuvitibu na rejesta. Miongoni mwa vihatarishi hivyo, nane (8) vinahusu Kurugenzi ya DMC, saba (7) vinahusu Kurugenzi ya DMD, na 11 vinahusu Vitengo chini ya Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu.

(e) Kufanya mapitio ya Sera ya Usimamizi wa Vihatarishi vya Udanganyifu (TMDA Fraud Risk Management Policy) ili kuendana na Mwongozo wa Uandaaji na Utekelezaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi vya Udanyanyifu kwenye Taasisi za Umma (Guidelines for Developing and Implementing Fraud Risk Management Policy in Public Entities) uliofanyiwa mapitio na Wizara ya Fedha mwaka 2023.

(f) Kuratibu maandalizi ya zoezi la ukaguzi wa nje wa mfumo wa uhakiki ubora wa huduma kwa mwaka wa fedha 2024/25 ambapo Mamlaka itakaguliwa kwa lengo la kuendelea kuthibitisha kuwa na mfumo thabiti wa uhakiki ubora wa huduma kwa mujibu wa kiwango cha ISO 9001:2015.

(g) Kufanya mapitio ya Mpango wa uendelezaji huduma wa mamlaka (Business Continuity Plan) na kuainisha na kufanya tathmini ya athari katika uendelevu huduma (Business Impact Analysis) katika michakato ya huduma za udhibiti zitolewazo na Mamlaka. Mpango husika umeidhinishwa na sasa hatua inayofuata ni kupima utayari wa utekelezaji wa mipango husika endapo majanga yatajitokeza.

(h) Kuratibu na kufanya ukaguzi wa ndani wa mfumo wa uhakiki ubora wa huduma (QMS Internal Audit) katika ofisi saba (07) za Kanda pamoja na vitengo/ sehemu kumi na tano (15) za ofisi za Makao Makuu kama moja ya matakwa ya kiwango cha ISO 9001:2015.

(i) Kuratibu mafunzo ya uelewa kuhusu mfumo wa uhakiki ubora wa huduma wa kiwango cha ISO 9001:2015 na usimamizi wa vihatarishi kwa watumishi wapya 45 na wasimamizi wa mifumo (QMS Champions) 28 walioteuliwa katika Vitengo, Sehemu na Ofisi za Kanda. Aidha, kupitia vipindi vya siku ya jumatano jumla ya vipindi 16 vya mafunzo mtambuka vimefanyika kwa watumishi wa Mamlaka hadi kufikia Juni 2025. Mahudhurio kwenye mafunzo haya yamekuwa na wastani wa watumishi 105 kwa kila kipindi, sawa na 25% ya watumishi wote, ambapo baadhi wanahudhuria kwa njia ya ana kwa ana katika ukumbi wa taasisi, na wengine kwa njia ya mtandao kupitia ***Zoom***.

(j) Kuteuliwa kwa watumishi 28 katika ngazi ya Kanda, sehemu na vitengo kuwa wakaguzi wa mdani wa mfumo wa uhakiki ubora wa huduma za Mamlaka.

(k) Kuratibu na kufanya ukaguzi linganishi wa ndani wa viwango vya udhibiti wa vifaa tiba, vitendanishi (Medical Devices Self Benchmarking Programme) kwa kushirikiana na Kurugenzi ya Vifaa Tiba na Vitendanishi (DMD). Aidha, Kitengo kinaendelea kufuatilia utekelezaji wa maboresho yaliyoanishwa na tathmini hiyo kama sehemu ya maandalizi ya ukaguzi rasmi unaotarajiwa kufanywa na Shirika la Afya Duniani (WHO) katika mwaka wa fedha 2025/26.

(l) Kuratibu zoezi la ukaguzi linganishi wa nje wa viwango vya mifumo ya udhibiti wa Damu na Mazao ya Damu (Blood and Blood Products Benchmarking Programme) kwa kushirikiana na Kurugenzi ya Vifaa Tiba na taasisi ya *Paul Ehrlich Institute (PEI)* ya nchini Ujerumani.

(m) Kuratibu mapokezi ya wageni waliokuja kwa lengo la kujifunza juu ya masuala ya ***Benchmarking*** kutoka nchi tano (5) za Zimbabwe, Msumbiji, Rwanda, Ethiopia na Ghana pamoja na Mamlaka ya Dawa na Chakula ya Zanzibar (ZFDA).

## 5.2 MIPANGO, UFUATILIAJI NA TATHMINI

Katika kipindi cha Julai 2024 – Juni 2025, Mamlaka ilikamilisha kazi zifuatazo: -

- Kuandaa na kukamilisha taarifa za utendaji kazi na tathmini za robo mwaka, nusu mwaka na taarifa ya mwaka 2024/25;
- Kuandaa na kukamilisha Mpango Kazi na Bajeti ya mwaka 2025/26; na
- Kufanya mapitio ya Bajeti ya mwaka 2024/25 ambayo yaliidhinishwa na MAB na kuanza kutumika mwezi Machi 2025.

## 5.3 TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA)

Mamlaka katika kuboresha na kutoa huduma kwa kutumia mfumo wa TEHAMA ilitekeleza kazi mbalimbali kama zilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 45**.

**Jedwali Na. 45: Mchanganuo wa Kazi za TEHAMA**

| Na. | Kazi | Utekelezaji | Kiwango cha Utekelezaji |
|---|---|---|---|
| **1** | **Kuimarisha Utendaji wa Masuala ya TEHAMA** | | |
| (a) | Kuratibu vikao vya Kamati ya TEHAMA | Kikao cha pili cha Kamati ya TEHAMA kilifanyika tarehe 29 Januari 2025 na kilijadili masuala yanayohusu TEHAMA | 100% |
| (b) | Watumishi wa TEHAMA kushiriki mafunzo | Jumla ya watumishi saba (7) kati ya saba (7) waliotarajiwa wameshiriki mafunzo ya TEHAMA katika eneo la Usalama wa mifumo na utengenezaji wa mifumo ya kielektroniki | 100%. Idadi ya watumishi walioshiriki mafunzo iliongezeka mwezi Juni, 2025 kwa kuwa mafunzo yalifanyikia katika Ofisi za TMDA. Mafunzo haya yaliendeshwa na Kampuni kutoka Kenya. |
| **2** | **Uboreshaji wa Mifumo ya Kieletroniki inayotumika na Mamlaka** | | |
| (a) | Mahitaji mbalimbali ya maboresho ya mifumo | Kupitia na kuainisha mapungufu ya moduli ya majaribio ya dawa ndani ya mfumo wa RIMS na kuandaa mahitaji ya kina ya utoaji wa taarifa ya viashiria vya utendaji kazi (KPI) | Kazi imekamilika. Hatua inayofuata ni kuanda muundo wa mfumo (System design) |
| | | Kuunganisha mfumo wa TANCIS na RIMS kwa ajili ya kubadilisha na taarifa za uingizaji vibali | Kazi imekamilika kwa 70%. Maeneo ambayo hayajakamilika ni:-<br><br>Kiunganishi (end-point) cha kutuma na kupokea hoja (Query Submission) kutoka mfumo wa RIMS kwenda TRA<br><br>Kiunganishi (end-point) cha kupokea matokeo ya ukaguzi wa pamoja katika vituo vya forodha (Joint Inspection at Port of Entry) |
| | | Kuandaa mfumo wa kukusanya taarifa za ukaguzi wa majengo kwa kutumia programu za simujanja (Android Apps) | Umekamilika kwa 100%. |
| | | Maboresho ya moduli ya PMS ndani ya mfumo wa RIMS kwa sampuli za vifaa tiba | |
| | | Maboresho ya mfumo upande wa GMP kwa ajili ya kupokea taarifa za viwanda vya ndani | |
| | | Kuzuia kufuta Ankara au malipo kwa ombi ambalo limefika hatua za mbele ndani ya mfumo wa RIMS | |
